WAEFESO

KWA WAUMIN WANAO KUA

5

Acknowledgments

The lesson outlines and notes in this booklet are based on New Tribes Mission's method of chronologically teaching scripture and were prepared by Tim McManigle, Director of FBC Missions and Scott McManigle.

Translated by Grace Outreach Mission (URIRI).

UTANGULIZI

WAEFESO KWA WAUMINI WANAO KUA
(Kiswahili Ephesians *for growing believers*)

	Ukurasa
Somo la 1	2
Somo la 2	9
Somo la 3	13
Somo la 4	18
Somo la 5	23
Somo la 6	28
Somo la 7	32
Somo la 8	35
Somo la 9	41

12/31/2010

WAEFESO KWA WAUMINI WANAO KUA- SOMO LA 1

A. Utangulizi.

- Kitabu hiki kiliandikwa na Paulo kwa kanisa la Efeso.
- Wakati wa kwanza Paulo alitembelea Efeso, yalikuwa ni matembezi yake ya pili ya kimisonari

19 "Wakafika Efeso, akawaacha huko.Yeye mwenyewe akaingia katika sinagogi, akahojiana na Wayahud.i 20 Hivyo ndivyo neno la Bwana lilivyozidi na kushinda kwa nguvu. 21 Mambo hayo yalipokwisha kumalizika, Paulo akaazimu Rohoni mwake, akiisha kupita katika Makedonia na Akaya, aende Yerusalem, akisema, Baada ya kuwako huko, yanipasa kuuona na Rumi pia. (Matendo ya Mitume 18:19,19:20 21)

- Paulo aliwatembelea tena katika Safari yake ya tatu wakati alikaa nao kwa miaka mitatu.
- Akiwa huko Efeso Paulo alivumilia mateso makali, ingawa watu wengi waliamini na kanisa likawa imara.

"Ikawa, Apolo alipokuwa Korintho, Paulo, akiisha kupita kati ya nchi za" juu, akafika Efeso; akakutana na wanafunzi kadhaa wa kadha huko;""Akaingia ndani ya sinagogi akanena kwa ushujaa kwa muda wa miezi mitatu akihojiana na watu, na kuwavuta katika mambo ya ufalme wa Mungu." Lakini wengine walikaidi, wakakataa kuamini, wakiitukana ile njia mbele ya makutano; basi, akaondoka akawaacha, akawatenga wanafunzi, akahojiana na watu kila siku katika darasa ya mtu mmoja jina lake Tirano. Mambo haya yakaendelea kwa muda wa miaka miwili, hata wote waliokaa (Matendo ya Mitume 19:1, 8-10)

Baadaye wakati Paulo aliporudi katika kanisa la Yerusalemu aliwaita wazee waje waonane naye kule meletus.

- Paulo aliwakumbusha mfano wake akawahimiza kutazama waumini wa Efeso kwa uaminifu na kanisa pia 17 ***"Toka Mileto Paulo akatuma watu kuenda Efeso akawaita***
- ***wazee wa kanisa, 18 walipofika kwake akawaambia,***
- ***Ninyi wenyewe mnajua tangu siku ya kwanza nilipokanyaga hapa Asia, jinsi nilivyokuwa kwenu wakati wote 19 nikimtumikia Bwana kwa unyenyekevu wote, na kwa machozi, na majaribu yaliyonipata kwa hila za Wayahudi 20 ya kuwa sikujiepusha katika kuwatangazia neno lo lote liwezalo kuwafaa bali naliwafundisha waziwazi, na nyumba kwa nyumba 21 nikiwashuhudia***

Wayahudi na Wayunani wamtubie Mungu, na kumwamini Bwana wetu Yesu Kristo. [22] ***Basi sasa, angalieni, nashika njia kwenda Yerusalemu hali nimefungwa rohoni, nisiyajue mambo yatakayonikuta huko;*** [23] ***isipokuwa Roho mtakatifu mji kwa mji hunishuhudia akisema, ya kwamba vifungo na dhiki vyaningoja.*** [31] ***Kwa hiyo Kesheni, mkikumbuka ya kwamba miaka mitatu, usiku na mchana sikuacha kumwonya kila mtu kwa machozi*** [32] ***Basi, sasa nawaweka katika mikono ya Mungu, na kwa neno la neema yake, ambalo laweza kuwajenga na kuwapa urithi pamoja nao wote waliotakaswa.*** [3 3] ***Sikutamani fedha wala dhahabu wala mavazi ya mtu.*** [34] ***Ninyi wenyewe mnajua ya kuwa mikono yangu hii imetumika kwa mahitaji yangu na ya wale waliokuwa pamoja nami.*** [35] ***Katika mambo yote nimewaonyesha ya kuwa kwa kushika kazi hivi imewapasa kuwasaidia wanyonge, na kuyakumbuka maneno ya Bwana Yesu, jinsi alivyosema mwenyewe, "Ni heri kutoa kuliko kupokea*** [36] ***Alipokwisha kunena haya akapiga magoti akaomba pamoja nao wote.*** [37] ***Wakalia sana wote, wakamwangukia Paulo shingoni wakambusu-busu,*** [38] ***wakihuzunika zaidi kwa sababu ya neno lile alilosema ya kwamba hawatamwona uso tena. Wakamsindikiza hata merikebuni*** **Matendo ya Mitume 20:17- 23, 31-38**

B. Paulo amekamatwa

- Baada ya Paulo kurudi Yerusalemu alikamatwa na kuwekwa gerezani kaisaria kwa miaka miwili baadaye alipelekwa Roma.
- Ulikuwa ni wakati alifungwa Roma ndio aliandika na kutuma barua hii kwa kanisa la Efeso. Roho mtakatifu alimuongoza kuandika barua hii, ulikuwa ni ujumbe kwa waumini wa efeso na kwetu sisi pia.

Paulo, mtume wa Kristo Yesu, kwa mapenzi ya Mungu; kwa watakatifu walioko (Efeso) wanaomwamini Kristo Yesu Waefeso1:1

- Kwa nini Paulo alijiita mtume? Tunasoma kwamba Paulo alikuwa ni mtume kwa mapenzi ya Mungu. Mungu alimchagua Paulo kuwa mtumwa wake, alitumwa kwenda kutangaza habari njema ya Yesu.
- Paulo hakuamua mwenyewe kuwa mtume bali Mungu ndiye alimchagua na kumtuma.
- Kumbuka nyuma katika kitabu cha Matendo ya Mitume wakati Mungu alimtuma Ananias kwa Paulo kule Damaskus. ***"lakini Bwana akamwambia, Nenda tu; kwa maana huyu ni chombo kiteule kwangu alichukue jina langu mbele ya mataifa, na wafalme na wana wa Israeli*** **(Matendo ya Mitume 9:15)**
- Kumbuka kwamba (**Waefeso 1:1)** pia inatuambia! Paulo alikuwa anaandika kwa watu gani; wateule wa Efeso.

- Paulo alitaja wateule wa Efeso kama “Waaminifu watiifu na wenye bidii ndani ya Kristo.” Paulo hakusema kwamba wateule wote wako hivyo lakini “ndani ya Kristo”, wameandaliwa na watawekwa waaminifu, watiifu na wenye bidii wakihudumia Kristo.
- Katika vitabu vingine vilivyo andikwa na Paulo kila mara alikuwa anataja waumini kama “wale wako ndani ya Kristo.” Mwanzoni tulikuwa ndani ya Adamu, lakini wakati tulitumainia Kristo Roho mtakatifu alitubatiza (kutuweka) ndani ya Kristo. Sasa mungu anatukubali vile anavyo kubali Kristo.
- Kukubaliwa kwetu na Mungu hakutegemei vile tulivyo ama yale tumefanya bali kunategemea yule ambaye tunamwamini.

Neema na iwe kwenu na amani zitokazo kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo. (**Waefeso 1:2**)

- Tazama mahali neema na amani zinatoka zinatoka kwa Mungu kupitia kwa kazi Yesu Kristo alifanya na kumaliza. Mungu tayari ametupatia neema na amani zote, na hatuyatambui haya wakati wote.
- Vile tunazidi kujua Mungu na kuelewa vyote tunavyo kwa Yesu, kwa hali halisi tutaanza kuzalisha na mwishowe kuwa na maisha ya neema na amani.

C. Baraka zote za Rohoni ndani ya Kristo

***“Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za Rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo. (*Waefeso1:3)**

- Paulo anasema “Atukuzwe Mungu” au “abarikiwe Mungu” kwa nini?
- Roho mtakatifu ametupatia baraka zote za Rohoni ambazo tunahitaji. Kwa sababu ya dhambi, mwili wetu unazeeka na kufa, na moyo na Roho vinatengwa kutoka kwa Mungu, na kuenda katika gehena milele.
- Kwa maana Kristo alikufa kwa ajili yetu, na tunamtumainia, Roho mtakatifu ana uwezo wa kutubariki na vitu vyote tunavyo vihitaji tukombolewe kutoka
- kwa hukumu ya dhambi na tena nguvu ya dhambi. Baraka hizi tunapewa na Roho mtakatifu na sio vitu vinavyo onekana kwa macho kama pesa, ngombe, gari na kadhalika.
- Watu wengi wanafikiria vitu vya dunia, (vitu vya muda kidogo) na wanataka wavipokee. Lakini hata kama tuko tajiri au maskini haijalishi tutakuwa na vitu vingi kiasi gani vya dunia tutakuwa navyo tu kwa muda mfupi tu.
- Nia yetu kubwa ingekuwa utajiri wa kiroho ambao tumepokea kutoka kwa Roho mtakatifu na utadumu nasi milele.
- Tazama kwamba Baraka hizi za kiroho tumepewa ndani ya Kristo kama Kristo angekufa na kufufuka kwa ajili yetu hatungepata baraka hizi za kiroho.

- Wakati tulikuwa ndani ya Adamu, tulipokea kutoka kwa dhambi ya Adamu na kifo; na sasa vile tuko katika Kristo, Roho mtakatifu ametupa maisha, na vitu vyote anavyo vimekuwa vyetu.

D. Tumechaguliwa ndani ya Kristo kuwa watakatifu.

[4] Kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo. **(Waefeso 1:4)**

- Tazama baraka ya kwanza Paulo ametaja ni Mungu ametuchagua ndani ya Kristo, hata kabla hajaumba chochote.
- Kwa maana Mungu anajua kila kitu, alijua kwamba binadamu angetenda dhambi na kwamba Mungu angetuma Yesu kufa kwa ajili yetu.
- Kwa hivyo, kwa hali yake ya kujua yajayo, alichagua wale ambao wangeokolewa kabla ya kuumbwa kwa dunia.
- Mungu alituchagua ndani yake kuwa watakatifu, bila lawana yoyote mbele yake. Kwa hivyo hata kabla hajaumba dunia Mungu alituchagua kutuweka ndani ya Kristo, ili kupitia kwa Kristo tuwe watakatifu bila lawama mbele yake, kumwezesha kutupokea.
- Hii Baraka ya kuwa mtakatifu na kuwa bila lawama tumepewa kuwa mahali pale kwa uwezo wa Roho mtakatifu.

[5]Kwa kuwa alitangulia kutuchagua ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi yake. (**Waefeso 1:5)**

- Baraka nyingine Paulo anataja hapa ni kwamba tumepata uridhi tuwe katika familia ya mungu kama watu wazima au watoto ili tusiwe na uoga wa kuhukumiwa. Na zaidi, kama watu wazima na watoto tuko na haki ya kudai uridhi wetu mara moja. (**Wagalatia 4:1-7)**
- Kama watoto wake, sisi ni warithi pamoja na Yesu, na vitu vyote anavyo na hali yake yote inakuwa yetu. **(Warumi 8:17)**

E. Tumekubaliwa kwa huyo mpendwa.

[6] Na asifiwe utukufu wa neema yake, ambayo ametuneemesha katika huyo mpendwa. **(Waefeso 1:6**)

- Baraka inayofuata ambayo Paulo anatufunulia ni kwamba tumekubaliwa na Mungu.
- Tulikataliwa na Mungu mara ya kwanza, kwa sababu tulikuwa wenye dhambi ndani ya Adamu lakini ndani ya Yesu ameturisha utukufu wake na kutufanya tukubaliwe na Mungu.

- Tukiwa peke yetu Mungu hawezi kutukubali, lakini Yesu ameturisha utukufu wake na kutufanya tukubaliwe na Mungu.

F. Tumekombolewa na kusamehewa

7 Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, msamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake **Waefeso 1;7**

- Baraka inayofuata kulingana na Paulo ni kwamba tume nunuliwa na damu yake, na tumesamehewa dhambi zetu, mstari huu unadhihirisha kwamba ndani ya damu ya Yesu ambayo ilitirika kwa ajili yetu, tumekombolewa na kusamehewa " kulingana na utajiri wa neema yake."
- Kulingana na utajiri wa neema yake" inamaanisha kwamba Mungu ametukomboa na kutusamehe kulingana na neema yake isiyo na upungufu ambao, Hakuna mwisho wa neema ya Mungu na yuko tayari kutupatia.
- Kwa hivyo, je kutakuwa na dhambi nyingi kuliko neema ya Mungu? Je tunaweza kutenda dhambi kiasi ambacho Mungu hawezi kutusamehe" sina neema ambayo imebaki kwako siwezi kukusamehe"? Hapana. Hakuna kipimo cha neema ya Mungu. Hatuwezi kutenda dhambi kiasi cha kufanya Mungu akose kutusamehe.

G. Kupewa uwezo wa kujua mpango ya Mungu yajayo

8 Naye alituzidishia hiyo katika hekima yote na ujuzi; 9 akiishia kutujulisha siri ya mapenzi yake, sawasawa na uridhi wake, alioukusudia katika yeye huyo. 10 Yaani, kuleta madaraka ya wakati mkamilifu atavijumlisha vitu vyote katika Kristo, vitu vya mbinguni na vitu vya dunia pia. Naam, katika yeye huyo **(Waefeso 1:8-10)**

- Baraka nyingine ambayo Paulo anataka tujue ni kwamba tumepata kuelewa ufunuo wa yale Mungu amefanya, anafanya na yale atafanya.
- Kabla hatujaokolewa tulikuwa tunaishi ndani ya giza. Sasa tuko na Roho mtakatifu ambaye atatufunulia ukweli kutoka kwa neno la Mungu.
- Sasa tunajua maisha ya milele na kitu ambacho kitafanyika kwetu tukifa.
- Tunajua kwamba Yesu ndiye kiini cha historia, na siku moja atarudi tena kwa watoto wake na kutuchukua tuwe naye milele.
- Tunajua ya kuwa sasa Shetani ndiye Bwana wa ulimwengu huu, ya kwamba siku moja atatupwa katika gehena milele, Ulimwengu huu utaangamizwa na mtawala wake.
- Tunajua haya yote kwa sababu Roho mtakatifu anatusimulia yote haya.

H. Tuliaidiwa uridhi na Bwana Yesu

“***Na ndani yake sisi nasi tulifanywa urithi, huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye, ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi yake.*** **(Waefeso 1:11)**

- Baraka inayo fuata ambayo Paulo anatuonyesha ni kwamba tumepata urithi ndani ya Kristo.
- Je watoto kutoka familia maskini wanapata urithi wazazi wao wakifa? La. Hakuna kitu cha kuwawachia.
- Wakati bado tulikuwa ndani ya Adamu tulikuwa kama watoto kutoka familia maskini. Hatukuwa na chochote kupokea isipokuwa kifo na gehemu.
- Sasa Mungu ametufanya watoto wake binafsi na tuko kama watoto wa mfalme tumepewa urithi wa kifalme, maisha ya milele upendo, kukubaliwa na kuwa na umoja na Baba.

[12] Nasi katika huyo tupate kuwa sifa ya utukufu wake, sisi tuliotangulia kumwekea Kristo tumaini letu; **(Waefeso 1:12)**

- Kwa sababu Mungu ametupa baraka hizi za kiroho; Teule, kuwa takatifu, kukubaliwa, nafasi ya kuwa watu wazima ambao ni wanawe, kukombolewa, kusamehewa, kufunuliwa hekima, kuwa warithi, tumepokea baraka hizi zote sio kwamba tulistahili kuzipata bali kwa sababu ya neema ya Mungu na upendo wake kwetu
- Tukiendelea kuwa kwa mawazo yetu kwa yale yote Mungu ametufanyia, Mungu atasifiwa mwishowe.

I. Kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu

[13] Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu wenu: tena mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu. **Waefeso 1:13**

- Paulo anatuambia kwamba baraka nyingine ambayo tumepata ni Roho mtakatifu. Mara tu tulipoanza kumtumainia Kristo, Mungu alitupa Roho mtakatifu.
- Mara kwa mara tuna tazama mali yetu ili tujue ni yetu ili mtu asiseme kwamba siyo yetu. Mungu ametununua na damu ya mwanawe na kutupatia Roho mtakatifu ambaye ametuweka muhuri na maisha ya Kristo.
- Shetani hawezi kutuchukua kama watoto wake kwa sababu tuko na Roho mtakatifu. Hii inahakikisha kwamba ni wana wa Mungu. Sisi ni wake.

J. Kukuja kwa Roho mtakatifu- Hakikisho ya ahadi ya Mungu kwa ukombozi yetu yajayo

***14 Ndiye aliye arabuni ya urithi wetu, ili kuleta ukombozi wa milki yake, kuwa sifa ya utukufu wake.* (Waefeso 1:14)**

- Paulo anasema hapa kwamba Roho mtakatifu siyo tu “Muhuri” unayo onyesha kwamba sisi ni wa Mungu. Bali yeye pia ni hakikisho kwamba sisi ni warithi. Wakati mwingine mtu akienda kununua kitu chenye thamani kubwa na hana pesa zote zinazohitajika, atawacha pesa kidogo kuonyesha mwusaji kwamba yuko na nia sana ya kununua kitu hicho, kitu hicho kitawekwa kando mpaka alipe pesa zote zilizobaki.
- Hata ingawa Yesu tayari amelipa gharama yote kwa dhambi zetu, bado tunaishi katika dunua hii ambayo imeanguka na miili iliyo laaniwa na urithi wetu wote hauja Dhihirika.
- Mungu alitupa Roho mtakatifu kuwa hakikisho kwamba tukipelekwa juu mbinguni mbali na ulimwengu, mbali kutoka miili hii tutapokea urithi wetu kwa kina. Kwa nafasi, tayari tumepewa urithi, na wakati bado tunaokaa katika ulimwengu huu unaoanguka na mwili ambao umelaaniwa, bado hatuwezi kuona urithi huo.
- Tukiwa huru katika maisha haya, na tuko pamoja naye, hapo tunaona vizuri mara ya kwanza vile Mungu ni wa ajabu <u>TENA</u> kubwa mno, mwenye huruma na upendo.
- Hili likitendeka, tutampatia sifa wa utukufu, hapo tutaona vizuri mara ya kwanza vile Mungu ni ajabu kubwa wa huruma na wa upendo.

WAEFESO KWA WAUMINI WANAO KUA- SOMO LA 2

A. Asante kwa Bwana kwa imani na upendo wa Waefeso

[15] Kwa sababu hiyo Mimi nani, tangu nilipopata habari za imani yenu katika Bwana Yesu, na pendo lenu kwa watakatifu wote. [16] Siachi kutoa shukrani kwa ajili yenu; nikiwakumbuka katika sala zangu. **(Waefeso 1:15,16)**

- Paulo alikuwa tayari amesikia kuhusu imani ya waefeso kwa Bwana, na upendo wao kwa wengine. (**Wakolosai 1:4 Warumi 1:8)**
- Waefeso walikuwa watu wa Mungu kwa kupitia kwa kifo cha Yesu.
- Sasa kila siku walikuwa wakiamini ahadi zote za Mungu kwa watoto wake.
- Walipozidi kusoma zaidi kuhusu nafasi yao ndani ya Kristo na kutembea kwa kutumainia Roho mtakatifu, upendo wa Mungu ukaanza kuteremka kupitia kwao kuenda kwa wengine.
- Waefeso walipenda wengine na pendo la Mungu ambalo ni tofauti na pendo la binadamu**. (1Wakorintho 13:4-7).**
- Upendo wa Mungu unapenda hata ingawa watu hawarudishi pendo lao. **(2 Wakorintho 12:15)** anapopenda adui wake matt 5:44
- Waumini waefeso walikuwa na upendo kama huu kwa sababu Roho mtakatifu, alikuwa anawadhihirisha kupitia kwao. Hawangetoa hilo peke yao.

B. Maombi ambayo itatupa Roho ya hekima na ya ufunuo katika kumjua yeye

[17] Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awape ninyi Roho ya hekima na ya ufunuo katika kumjua yey*e.* **(Waefeso1:17)**

- Waumini Waefeso walikuwa na imani na upendo kwa wengine, Lakini Paulo aliomba ili Mungu ajidhihirishe kwao ili wamjue kwa undani zaidi. Kama watoto wa Mungu, hayo ndiyo mahitaji yetu muhimu. "*Swala kubwa zaidi mbele ya Kanisa ni Mungu mwenyewe, na jambo linalo ogofya juu ya binadamu yeyote sio yale anaweza kusema au kufanya lakini ni vile anavyo jua na kuelewa Mungu kutoka ndani ya moyo wake--- Kila mara kinacho jidhihirisha kumhusu ni vile anavyoelewa Mungu tena kilicho, muhimu kwa kanisa ni yale anayosema kumhusu Mungu au yale amewacha kusema kumhusu Mungu kwa kuwa kunyamaza kwake kuna zungumuza zaidi kuliko hutuba --- kwa hakika makosa ya ujumbe wowote au kukosa kutumia maadili ya ukristo unaweza kuelezwa kama mawazo duni kumhusu Mungu ---Yule ambaye anakuwa na amani sawa kumhusu Mungu anapungukiwa na maelfu na maelfu ya matatizo hayo yanahusu ambayo kwa uzuri huwezi kumhusu kwa muda mrefu". (Mwandishi hajulikani kwangu)*

- Hatutaki imani zaidi, upendo zaidi, huduma zaidi bali tunahitaji kumjua Mungu zaidi na zaidi. Tukizidi kumjua ndivyo tutakuwa na imani, upendo na kutoa huduma.
- Tulipo okolewa, Mungu alitupatia nafasi ya kuwa watoto wazima, na kila mara hatuonekani kutenda kazi kama watoto wazima kila mara tunaonekana kama watoto ambao ni matokeo ya kutokumjua.
- Je unatarajia mtoto wako mchanga kuwa kama mtu mzima? Hapana, kwanza mpaka wachukue muda wao wa utotoni kusoma na kukuwa kwa miaka mingi kabla hawaja kuwa watu wazima.
- Hata sisi mpaka tusome na tuwe kwa mawazo yetu na hekima ya Mungu kabla kuanza kuwa kama watoto wazima wa Mungu.
- Kazi ya Roho Mtakatifu ni kumdhihirisha Mungu kwetu. Hatuwezi kusoma kumhusu peke yetu, hatuwezi kusoma kumhusu hata tukisoma Biblia.
- Lakini Paulo aliomba kwamba Mungu angejidhihirisha kwao ili wamjue kwa kina zaidi. Kutojali kwa nguvu kuliko kuwapenda na kwa uangalifu, kwa wale ambao wana ogofya na
  tukitilia maanani kwamba Biblia iliandikiwa na Roho mtakatifu, kwa hivyo inaweza kueleweka tu kiroho. Roho wa ukweli pekee ndiye anaweza kueleza Mungu kwe[12]
- Mpaka tutumainie Roho mtakatifu kuchukua neno la Mungu na kutufundisha moyoni kutufunulia ukweli wa Mungu zaidi na zaidi.

***[16] Nami nitamwomba Baba, naye atawapa msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele [17] ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui ; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu [26] basi Yesu akajibu, ndiye mtu yule nitakaye mtoleo tonge na kumpa. (*Yohana 14:16,17,26) *[12] Hata bado ningali ninayo mengi ya kuwaambia lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa [13] lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe lakini yote atakayoyasikia atayanena na mambo yajayo atawapasha habari yake.* (Yohana 16: 12-14)**

- Roho mtakatifu alitumwa kuishi ndani yetu kutuongoza kwa ukweli wa neno la Mungu.
- Mpaka tumtumainie kufanya yale Mungu alimtuma kufanya.

C. Mjue tumaini la mwito wake jinsi lilivyo

***[18] Macho ya mioyo yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la mwito wake jinzi lilivyo; na utajiri wa utukufu wa urithi wake wa katika watakatifu jinsi ulivyo. (Waefeso 1:18*)**

- Paulo aliomba ili macho yao yafunguliwe waone tumaini la mwito wake. Tilia maanani kwamba mwito wa Mungu kwanza ni kwake mwenyewe **(**Wakorintho 1:9: Math 4:18-20; Mk 3:13-14; Mk 6:7) kama mitume, Mungu kwanza anatuita kwake baadaye anafanya kazi ya ajabu kwa maisha yetu, kutuumba kwa sura ya mwanawe baadaye anatutuma nje kwa nia yake kutimiza mpango wake.
- Tumepewa maisha yake. Maisha ya Kristo.
- Roho anapenda kutuonyesha Kristo, na baadaye anazalisha maisha yake kwetu na mwisho kudhihirisha maisha yake kwetu kila siku.
- Mungu pia anatuita kwa maisha ya milele tuwe naye. Tulipookolewa tulipewa hakikisho moyoni mwetu kwamba yesu ametupa maisha ya milele na kwamba siku moja atatupeleka mbinguni tuwe naye.

D. Maombi kwamba watajua utajiri ya utukufu wa uridhi wa Mungu kwa wateule

- Paulo pia aliomba ili macho yao yafunguliwe kwa “utajiri wa utukufu wa urithi kwa wateule” Mstari huu hauonekani kama unazungumuzia urithi wetu ndani ya Kristo kama vile imeandikwa kwenye mstari wa 11, bali ni urithi wake ndani yetu. Ni kitu cha ajabu kwamba Bwana anatutazama kama baadhi ya mali yake kuu. (Kumbu 32:9-19)

E. Maombi kwamba watakuwa na uwezo kujua ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tunaamini

[19] Na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake [20] aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa Roho.
(**Waefeso 1:19-20**

- Jambo la mwisho Paulo aliwaombea ni Mungu kudhirisha nguvu zake kuu ambazo Roho mtakatifu anapendelea kuonyesha kupitia kwetu na pia ndani yetu. (**Wokolosai 1:11)**
- Vitu ambavyo tunatarajia, kama uokovu, maisha ya milele na kadhalika, vitakuwa upumbavu kwa wasioamini, na kwetu vitu hivi sio upumbavu. Tunajua kwamba baada ya Yesu kufa kwa ajili yetu na kuzikwa Mungu alimfufua akawa mzima tena na kumchukua mbinguni.
- Kwa maana hii ilifanyika kwa Yesu na sasa vile “tuko ndani yake” tunao ujasiri kwamba Mungu anaweza na atafanya yote ambayo alituahidi katika neno lake.
- Mpaka tutumainie roho mtakatifu atuonyeshe mengi zaidi kuhusu vile nguvu zake ni kuu na kwamba anafanya kazi ndani yetu, na kwetu.
- Tunavyozidi kumwelewa Mungu na kumwelewa ndivyo tunavyomtumainia.

F. Kuinuliwa kwa nafasi ya Bwana Yesu Kristo

21 Juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu bali katika ule ujao pia (Waefeso 1:21)

- Paulo anatuambia kuhusu nafasi ya juu iliyo inuliwa ambayo yesu alipata baada ya kufufuka kutoka kwa wafu na kuenda mbinguni. **(Walilipi 2:9-11)**
- Yesu ameinuliwa juu ya 15 alaika, shetani na malaika wake wachafu na watu wote mahali popote milele.
- Ni muhimu tujue nafasi ambapo Mungu ameinua Yesu kwa maana hapo ndipo Biblia inasema ya kwamba tunakaa na yeye. **(1Wakorintho 1; 30)** tunasoma "kwa yeye, ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu" Mungu alituchukua na kutuweka ndani ya Kristo. Wakati Yesu alienda msalabani, tulienda msalabani na yeye, wakati alienda kaburini, tulienda kaburini naye, na wakati alipaa juu katika mkono wa kiume wa Mungu (Baba) na hapo ndipo nafasi yetu ndani yake.
- "***22 Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo 23 ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.*** **(Waefeso 1:22-23**)
- Kanisa ni mwili wa Yesu na yeye ndiye kichwa.
- Hii inamaanisha kwamba Yesu ndiye mwenye mamlaka yote juu ya kanisa lake na pia ni ukamilifu wetu sote vile Roho mtakatifu anatujaza na maisha yake.

WAEFESO KWA WAUMINI WANAO KUA- SOMO LA 3

A. Makumbusho

- Katika somo la 2 Paulo aliwaambia Waefeso walioko ndani ya Kristo. Sasa kwa juhudi za kueneza neema ya Mungu kwa yale yote ambayo wamepewa, Paulo aliwakumbusha vile walivyokuwa wakati walipo kuwa ndani ya Adamu 1 Ninyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu **Waefeso 2:1**
- Kabla ya kuokolewa, kusimama kwetu mbele ya Mungu kulikuwa kwa kifo na kugawanyika. Tulizaliwa hapa duniani tukiwa ndani ya Adamu tukitengana na Mungu tukiwa kwa njia ya kwenda ahera milele.
- Ingekuwa vizuri kutazama (**Warumi 5:12)** na (**Warumi 6:23)** kwa sababu ya dhambi ya mtu mmoja (Adamu) sisi sote tulizaliwa wenye dhambi na tulikuwa chini ya nguvu za kifo.
- “Mshahara wa dhambi ni mauti” tulizaliwa wenye dhambi
- Wakati huo, hata ingawa mwili wetu ulikuwa na uhai, kiroho tulikufa, na kutengana na Mungu na kuwa njiani, kwenda gehena.
- Mwanzoni Mungu aliumba binadamu akiwa mkanilifu na bila dhambi na wakati Adamu na Hawa walitenda dhambi wajukuwao wote walizaliwa wenye dhambi na walikuwa wamekufa mbele za Mungu.

B. Vile tulivyo apo awali.

“*Ambazo mliziendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, na kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga, Roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi.* (Waefeso 2:2)

- Katika mstari huu, Paulo ametaja vitu vitatu ambavyo vinaonyesha maisha ya wasio amini ambao wako chini ya mamlaka ya kifo.
- Kwanza, anasema tulikuwa tukitembea kwa njia ya ulimwengu huu.
- Hii inamaanisha ya kwamba tulikuwa katika uongozi wa ulimwengu huu, na hali yake na nguvu za Kishetani kama, ulafi, tamaa kutembea na kukubali njia ya uovu.
- Hatukuwa tunatembea kwa njia za Mungu.
- Pili Paulo anasema: tulitembea kulingana na nguvu ya ufalme wa anga.
- “Ufalme wa nguvu za anga” inamaanisha Shetani.
- Kwa kuwa tulitengana na Mungu kutembea kwa njia ya ulimwengu huu na kwa vile Shetani alikuwa anaongoza njia ya ulimwengu huu tuko chini ya mamlaka haya, tukiongozwa na uongo wake.
- Tatu, Paulo anasema tulitembea tukiongozwa na Roho inayofanya kazi katika maisha ya wanaoasi.

- Vile tulikuwa tukitembea kulingana na njia ya ulimwengu huu na kuwa chini ya utawala wa Shetani tulikuwa hatuko tofauti na wengine wengi ambao hawajui Mungu. Tulitembea tukiasi Mungu.

C. Watoto wa laana

[3] ambao zamani, sisi sote nasi tulienenda kati yao, katika tamaa za miili yetu tulipoyatimiza mapenzi ya mwili na ya nia, tukawa kwa tabia yetu watoto wa hasira kama na hao wengine. **(Waefeso 2:3)**

- Kwa sababu tulizaliwa ndani ya Adamu, kutengana na Mungu tuliishi kwa uongozi wa mara kwa mara ya miili yetu ambaye ni tamaa ndani yetu ya kufanya mabaya.
- Yote ambayo miili yetu inatamani ni dhambi, na vile tulikuwa tunaishi chini ya uongozi wake alikuwa akiongoza fikira,
  nia na tabia yetu ambayo inasababisha kuongozwa kwa miili yetu, tabia yetu (Mahali tunaenda kile tunasikiliza, yale tunaangalia na yale tuna sema NK.)
- Kwa sababu tulizaliwa ndani ya Adamu kutengana na Mungu chini ya uongozi wa shetani na kutembea chini ya uongozi wa mwili, Paulo anasema kwamba tulikuwa watoto wa hasira ya Mungu.
- Hatukuzaliwa tu kutengana na Mungu, lakini tulizaliwa kupokea hasira yake kwa dhambi na kumkataa. (**Warumi 1:18**)
- Hii ndiyo hali na nafasi kila binadamu amezaliwa
  (a). Kutengana na Mungu.
  (b). Chini ya mamlaka ya Shetani.
  (c). Kuishi chini ya Uongozi wa mwili.
  (d). Watoto wa hasira.

D. Nafasi ya zamani na mpya.

[4] Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda [5] hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo yaani, tumeokolewa kwa neema [6] Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa Roho, katika Kristo Yesu. (Waefeso 2:4-6)

- Nafasi yetu ya zamani katika Adamu ilikuwa haina tumaini, tulikuwa watu bila tumaini.
- Tulikuwa kama Jona wakati alikuwa ndani ya tumbo ya samaki. Kwake mwenyewe hakukuwa na tumaini la kuponyoka. Kama Mungu hangefanya kitu kumwokoa Jona angekufa na hange okolewa.

- Hivyo ndivyo tulivyo kuwa wakati bado tulikuwa ndani ya Adamu, kama Mungu hangefanya kitu kutuokoa, sisi sote tungekufa kwa dhambi zetu na kwenda gehena kuhukumiwa milele.
- Hakuna njia yoyoye ambayo tungetumia kujiokoa.
- Lakini Paulo anasema kwamba Mungu ana utajiri mwingi wa huruma na anatupenda kwa pendo kuu. Anahuruma sio “kupata kile ambacho tunastahili” sisi tulistahili gehema lakini Mungu alitupa maisha ya milele mbinguni tuwe naye.
- Tunaweza kuchukua muda kufikiria picha ambayo Paulo anaeleza hapa.
- Tulizaliwa wenye dhambi, kutengana na Mungu tulikuwa adui wake chini ya mamlaka ya shetani tukiongozwa na mwili. Tulikuwa watoto wa hasira ya Mungu kuelekea katika gehena.
- Lakini Mungu ambaye ni tajiri hapatii binadamu yale ambayo anastahili, na kwa sababu ya upendo wake mkuu anao kwetu, alitufanya wazima pamoja na Kristo.
- Neema ya Mungu na upendo ulikuwa ni mikuu hakutuwacha tukiwa tumetengana naye.
- Sheria ya Mungu inahitaji dhambi ili ihukumiwe lakini Neema na Upendo haviwezi kuturuhusu kubeba hukumu huo sisi wenyewe ilimfanya kutuma mwanawe kutubebea hukumu huo ili tukombolewe tuwe pamoja naye.

[6]Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa Roho, katika Kristo Yesu. **(Waefeso 2:6)**

- Hiki ndicho kitu ambacho Paulo aliandika nyuma katika Warumi 6 pahali alisema kwamba, kwa sababu ya Yesu kutukufia na kwa maana kwamba tumewekwa ndani ya Kristo na Roho mtakatifu vitu vyote ambavyo vilifanyika kwake vilifanyika kwetu pia.
- Alisulubiwa, tulisulubiwa pamoja na yeye.
- Alizikwaa, kafufuka na kupaa kuwa upande wa kulia wa Baba sisi pia tumefufuliwa ili tutembee kwa maisha ya umoja **(Warumi 6:4)** ya mtazamo mpya ambayo yanatokana na nafasi yetu mpya katika mkono wa kulia wa Baba.
- Ingawa Mungu anasema kwamba sisi ambao tuko ndani ya Kristo hatupaswi kuwa na tabia kama hizo.
- Hiyo ni kwa sababu mfululizo wa tabia zetu za kila siku unakaa na thamani kulingana na nafasi yetu mpya. Kukua huku kunachokua muda mrefu na kunaenda pole pole, na Roho mtakatifu ndiye anatekeleza hayo katika maisha yetu yote. Kukubali pendo lake tukiwa bado hatuna thamani ni taaabu kubwa kwetu.
- Kiwango hiki kinaanza na hekima. Kwanza roho anaanza kutuonyesha vitu ambavyo ni vyetu na vile tulivyo ndani ya Kristo. Basi Roho zetu zinasawishika

na ukweli huu. Tunaamini ukweli ambao umeaminiwa utazalisha maisha kama ya Kristo.

E. Neema ya milele

***[7] ili katika zamani zinazokuja audhihirishe wingi wa neema yake upitao kiasi kwa wema wake kwetu sisi katika Kristo Yesu.*" (Waefeso 2:7)**

- Paulo ananena kwamba kitu ambacho Mungu amekamilisha kwetu, ndani ya Kristo iktaonyesha neema kuu ya ajabu, neema yake ni ya milele.
- Tia maanani kwamba neema ni “mapendeleo tusiyo stahili” kumpatia mtu kitu ambacho hastahili kupata.
- Katika historia yetu ya binadamu, hakuna kitendo ambacho mtu alikuwa anastahili kupata kitu ambacho wamepata, kama vile tulivyo kuwa wakati Mungu alituma mwanawe kufa kwa ajili yetu.
- Kufikiria haya kutafanya vitu viwili: Kutaonyesha utukufu wa neema ya Mungu na hali ya Adamu. Mungu asifiwe kwa neema yake.

F. Utajiri katika Huruma

***[8] Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu [9] wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.* (Waefeso 2:8, 9)**

- Hakuna mkristo ambaye amezaliwa upya ambaye amewahi kuishi ambaye angestahili kupata uokovu waliopata ndani ya Kristo.
- Sio Abeli, Seth, Enoka, Noah, Abrahamu, Isaka, Jakobo, Yosefu, Musa, Daudi, Maria Yohana mbatizaji, hakuna hata mmoja wa mitume wa Yesu hata sio wewe ama mimi, hakuna hata mmoja angestahili kuokolewa wote waliostahili hukumu wa milele katika gehena.
- Lakini Mungu amejaa huruma na kwa ajili ya upendo wake mkuu kwetu sasa tumekombolewa kutoka kwa dhambi, na hukumu yake pia na nguvu zake na tumewekwa watoto watakatifu wenye haki wa Mungu.

G. Kutembea kwa matendo

***[10] Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo.* (Waefeso 2:10)**

- Kumbuka nyuma katika mstari wa 1-3 Paulo anasema vile nafasi yetu ya zamani ndani ya Adamu ilivyo kuwa, pamoja na vitendo ambavyo vilitokana nayo.

- Mstari wa 4-9 Paulo anaona nafasi yetu mpya ndani ya Kristo ni kwa ajili ya neema ya Mungu.
- Sasa katika mstari wa 10 Paulo anataja matunda ya nafasi yetu mpya- matunda mema.
- Kwa kiwango kile tunamjua, kumuelewa na kwa imani kupokea na kupumzika kwa nafasi yetu mpya ndani ya Kristo tutatembea kwa matendo mema.
- Kwa maana vile dhambi ni matokeo ya mwili, ndio vile matendo mema ni matokeo ya nafasi yetu mpya na uhusiano wetu na Kristo

WAEFESO KWA WAUMINI WANAO KUA- SOMO LA 4

A. Kulinganishwa kwa hali ya kale na hali mpya

- Paulo analinganisha hali ya kale katika Adamu na hali mpya tumepokea katika Kristo.

[11] Kwa ajili ya hayo kumbukeni ya kwamba zamani ninyi, mlio watu wa mataifa kwa jinsi ya mwili, mnaoitwa wasiotahiriwa, na wale wanaoitwa waliotahahiriwa, yaani, tohara ya mwili iliyofanyika kwa mikono. (**Waefeso 2:11)**

- Kutahiriwa kwa wayahudi kulikuwa muhimu zaidi, vile ilivyokuwa ni dalili ya kwamba walikuwa juu ya watu wa dunia, tena walikuwa wateule wa Mungu.
- Kwa sababu walichaguliwa na Mungu na si wayahudi hawakuchaguliwa, walidharau wasiokuwa wayahudi kuwatazama kama watu waovu.

[12] Kwamba zamani zile mlikuwa hamna Kristo mmefarakana na jamii ya Israeli, wageni wasio wa maagano ya ahadi ile. Mlikuwa hamna tumaini, hamna Mungu duniani. [13] Lakini sasa, katika Kristo Yesu, ninyi mliokuwa mbali hapo kwanza mmekuwa karibu kwa damu yake Kristo. **(Waefeso 2:12,13**

- Paulo anawakumbusha waumini waefeso kuhusu hali yao ya kale, kutengana na Kristo na kuwa nje katika jamhuri ya Israeli na wageni kwa agano la ahadi.
- Waisraeli walikuwa na tumaini la ahadi ya mkombozi lakini wasio kuwa waisraeli walitengana kwa hayo yote.
- Katika agano la kale lote, Mungu aliwahifadhi, kuwatazama na kuwabariki waisraeli. Aliwapa njia kila mara ya kuwafanya wakubaliwe naye.
- Na wasio kuwa Waisraeli hawakukuwa na hayo yote, mema ni matokeo ya nafasi yetu mpya na uhusiano wetu na Kristo
- Wasiokuwa Waisraeli hawakumjua Mungu, agano lake, ahadi ya mkombozi ambaye angekuja kufungua watu kutoka kwa dhambi zao
- Sisi pia sio Waisraeli, na tulitengana na Kristo, tena tulikuwa wageni kwa agano la ahadi ya Mungu.
- Lakini Paulo anaendelea kusema kwamba ingawa sisi pamoja na waefeso, mara ya kwanza tulikuwa mbali kuwa na uhusiano na Mungu na ahadi zake, sasa tumeletwa karibu na damu ya Kristo.

"[14] Kwa maana yeye ndiye amani yetu, aliyefanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja; akakibomoa kiambaza cha kiti kilicho tutenga. [15] Naye akiisha kuuondoa ule uadui kwa mwili wake; ndiyo sheria ya amri zilizo katika maagiz;o ili afanye hao wawili kuwa mtu mpya mmoja ndani ya nafsi yake **(Waefeso 2:14-15)**

- Chini ya sheria wayahudi walikuwa na haki ya binafsi, waki hukumu wasio kuwa waisraeli kwa maana hawakuwa wanafuata sheria, kati ya Waisraeli na wasiokuwa Waisraeli.
- Na sasa katika Kristo Mungu anavunja kiambaza cha kitu kilicho watenga cha uadui iliosababishwa na sheria.
- Sasa sheria haina kazi ndani ya Kristo, wayahudi hawana chochote cha kujisifu isipokuwa neema ya Mungu, kwa hivyo walikuwa na nafasi kujitukuza kuwa wenye haki ya kibinafsi.
- Kwa ajili ya Kristo watu wote duniani wako sawa. Wale ambao wamekubali Kristo kuwa mwokozi wao, na wale wamemkataa wanabaki wakitengana na Mungu wakiwa wayahudi au wasio kuwa Wayahudi.

[16] Akawapatanisha wote wawili na Mungu katika mwili mmoja, kwa njia ya msalaba, akiisha kuufisha ule uadui kwa huo msalaba [17] Akaja akahubiri amani kwenu ninyi mliokuwa mbali, na amani kwao wale waliokuwa karibu [18] Kwa maana kwa yeye sisi sote tumepata njia ya kumkaribia Baba katika Roho mmoja. **(Waefeso 2:16-18)**

- Awali waisraeli walikuwa watu walioteuliwa na Mungu na watu wengine wote hawakuteuliwa, lakini sasa, kupitia kwa msalaba tuko na njia kwa Roho kwa Baba kama watoto wake, na wale ambao ni watoto wa Mungu wako katika mwili mmoja na Kristo.
- Leo, ndani ya Kristo sote tuko na njia kwa Mungu kupitia kwa Roho. Yeye ndiye Baba wetu wa mbinguni na tunaweza kwenda kwa kiti cha enzi cha neema wakati wowote (**Waebr 10:19)**
- Kabla ya Kristo kuja na kuwezesha haya, Mungu angeabudiwa katika hekalu na kwa sheria iliyo wekwa.
- Hakuna mtu ambaye hakutahiriwa asiye kuwa Mwisraeli angeingia na wayahudi katika chumba cha ndani cha hekalu.
- Ingawaje, wakati Yesu alikufa msalabani na kulia kwa sauti “imekwisha” kitambaa katika hekalu kiliraruka kutoka juu hadi chini, ambayo ilikuwa ishara ya Mungu kwamba, sasa kupitia kwa Kristo watu wote watakuwa na nafasi na njia ya kuenda kwa Mungu Baba.

[19] Basi tangu sasa ninyi si wageni wale wapitaj, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu [20] Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni. [21] Katika yeye jengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho. (**Waefeso 2:19-22**)

- Wakati wa agano la kale, mahali pa kuishi pa Mungu ulimwenguni palikuwa ni Hema (tabernacle), na baadaye pakawa ni hekalu wayahudi waliojenga kwa mawe.
- Lakini leo, mahali pa kuishi pa Mungu duniani ni ndani ya wale ambao wamekuwa watoto wake.
- Roho imetuweka pamoja “ndani ya Kristo” Paulo anasema tunakuwa kama hekalu takatifu “ndani ya Bwana”

B. Kupewa nguvu na Roho.

14 Kwa hiyo nampigia Baba magoti, 15 ambaye kwa jina lake ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa, 16 awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani. ***(*****Waefeso 3:14-16)**

- “Kwa kadiri ya utajiri utukufu wake” weka maanani kwamba (**Kutoka 33;18)** Musa alimwomba Mungu kumwonyesha utukufu wake na Mungu akamjibu katika mstari wa 19 “nitapitisha wema wangu wote mbele zako” na tena katika (**Kutoka 34;6)** alieleza kwamba utukufu wake ni, neema huruma na mapenzi kwa mtu mwenye dhambi.
- Paulo aliomba kwamba Wakristo wangepata nguvu kutokana na nguvu zake ambazo ni wema wake.
- Kuna kiwango cha utajiri wa utukufu wa Mungu? La tena hakuna kiwango cha nguvu ambacho Mungu anatupa (**Wakolosai 1:11)**
- Sababu inayotufanya kuwa wanyonge kama wakristo ni kwa sababu ya mwili, kwa kiwango kile tunatembea kwa mwili hatuwezi kuwa na hujuzi kwa nguvu ya Roho ndani yetu (**Wagalatia 5:16)**
- Tukizidi kutembea kwa Roho, tutazidi kuwa na nguvu zake, maishani mwetu **2Wakorintho 3:17-18**

17 Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo 18 ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; 19 na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutumikia kwa utimilifu wote wa Mungu. **(Waefeso 3:17-19**)

- Paulo anapo omba kwamba wakati Kristo anazaliwa ndani ya Roho zetu kwa imani tutaanza kuelewa upana wa pendo lake kwetu na kuwa imara katika pendo lake.
- Tukizidi kukua katika kuelewa upeo wa pendo lake kwetu tutavutwa karibu naye tukijazwa na uwezo wote wa Mungu”

- Tukizidi kutembea kwa Roho, ndivyo Roho itatujaza na maisha ya Kristo ambayo ni ukamilifu wa Mungu

[20] Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu [21] naam atukuzwe katika kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya milele na milele. Amin. (Waefeso 3:20)

- **Efeso 3;20-21)** huwa inatajwa kuhusu mahitaji ya binadamu ya dunia na zaidi ya hayo linakuwa somo lenye ukweli mkubwa kwetu kutazama
- Paulo anasema kuhusu kazi ya kufanya binadamu kuwa katika sura ya Kristo, mpaka ajazwe na ukamilifu wa Mungu, sio tu kwamba Mungu anauwezo wa kukamilisha maisha yetu kwa Kristo kwa
  wingi zaidi kiwango ambacho hatuwezi kufikiria.
- Nguvu na mamlaka hiyo moja ambayo ya ilimfufua Kristo kutokana kwa kifo, na kumkalisha mkono wa kiume wa Mungu, ndiyo ambayo wakati wa leo unafanya kazi ndani yetu, kutuweka imara katika kukuwa kwetu pamoja na Kristo, hivyo basi kutufanya zaidi kuwa katika sura yake.
- Tukikumbuka mara kwa mara vita vilivyoko kati ya mwili na Roho. (**Wagalatia 5:17)**
- Tukihesabu kwa imani kusulubiwa kwetu na Kristo, tuko huru kutokana na kuongozwa kwa mwili, bali tukaongozwa na Roho mtakatifu.
- Tukizidi kutembea kwa Roho (kuhimizwa na kuongozwa) ndivyo tutazidi kuwekwa katika sura ya Kristo, tukijazwa zaidi na Roho na maisha ya Kristo, na ndivyo tutapata utukufu ndani na katika maisha yetu **(2 Pet 3:18)**

[15]Basi angalieni sana jinsi mnavyoenenda; si kama watu wasio na hekima bali kama watu wenye hekima; [16] mkiukomboa wakati kwa maana zamani hizi ni za uovu. [17] Kwa sababu hiyo msiwe wajinga, bali mfahamu ni nini yaliyo mapenzi ya Bwana. (**Waefeso 5:15-17)**

- Tunajua kwamba tumepewa maisha mapya ndani ya Kristo. Tena tunajua kwamba Kristo anatupenda, na ametupa Roho Mtakatifu kutuongoza kwa maisha ya kupendeza ya Mungu.
- Kwa hivyo simama na utembee na kuishi kwa imani, kwa ukweli huu, sio kutembea kama wale ambao hawana vitu hivyo.
- Ulimwengu unaelekea kutoka kuwa mbaya na kuwa mbaya zaid, ina muda unaendelea kuyoyoma, kwa hivyo, tungetembea kila mara tukitumainia Roho Mtakatifu kutuonyesha mapenzi yake kwa wakati wake.

[18] Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho; [19] Mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za Rohoni, huko mkiimba na

kumshangilia Bwana mioyoni mwenu; na kumshukuru Mungu Baba siku zote kwa mambo yote, katika jina lake Bwana wetu Yesu Kristo; [21] hali mnanyenyekeana katika kicho cha Kristo. (**Waefeso 5:18-21)**

- Angekuwa ni Roho mtakatifu ambaye angetuongoza na vitendo vyetu, sio pombe, dawa ama vitu vingine.
- Tukitembea kwa mwili, tamaa nyingine nyingi za kimwili kama dawa za kulevya, pombe tamaa mbaya, ulafi kupenda mali ya dunia mamlaka N.K. zitatuongoza na sio Roho mtakatifu.
- “Kujazwa na Roho” ni hali ya maendeleo na kwa hakika kujazwa na Roho ina maanisha kwamba Roho anatujaza na maisha ya Kristo.
- Ushahidi wa kwanza unakuja kwetu “mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za Rohoni” moyo mwepesi wenye furaha na amani kwa Mungu
- Ushahidi wa pili inaenda kwa Mungu “kumshukuru Mungu Baba siku zote kwa mambo yote katika jina lake Yesu Kristo.
- Ushahidi wa tatu ni kwa wenzetu kunyenyekeana katika hicho cha Kristo (hekima kuu) ya Mungu
- Tukijazwa na Roho kujazwa na maisha ya Kristo mioyo yetu itajazwa na furaha na shukrani kwa Bwana. Ikiwa wanao tuzunguka, wanaona kwamba furaha na shukrani hiyo Roho mtakatifu itaitumia kuiweka imara na kuhimiza Roho zetu vizuri.
- Wale ambao wanahimizwa na kuongozwa na Roho mtakatifu wana uwezo wa kunyenyekea kwa wengine kwa maana wanapumzika kwa wema na utukufu wa Mungu.

WAEFESO KWA WAUMINI WANAO KUA- SOMO LA 5

A. **Wakristo kuishi pamoja kwa umoja**

[1] Kwa hiyo nawasihi, mimi niliye mfungwa katika Bwana, mwenende kama inavyoustahili wito wenu mlioitiwa (**Waefeso 4:1)**

- Paulo alikuwa mfungwa katika Roma wakati alikuwa anaandikia waumini wa Efeso, ingawaje, ya muhimu zaidi aliona kwamba alikuwa mfungwa, kutekwa nyara na Yesu Kristo.
- Katika sura tatu za kwanza za barua yake Paulo anawafundisha waumini wa Efeso vitu ambavyo ni vyao kiroho "ndani ya Kristo"
- Tumepokea kila baraka ya kiroho, tumechaguliwa, ametuchukua kama watoto wake, tumekubaliwa, tumekombolewa na kusamehewa, tumepewa urithi na hakikisho la Roho mtakatifu (**Waefeso 1:3-4)**
- Na zaidi waumini wote wamewekwa pamoja na Kristo mbinguni, (**Waefeso 2:5,6)** na wamekuwa hekalu la Mungu ambamo anaishi kupitia kwa Roho Mtakatifu **(Waefeso 2:22)**
- Sasa katika Waefeso 4, Paulo anatujulisha kwamba kwa ajili tumebarikiwa na baraka hizi za kiroho ndani ya Kristo sasa inawezekana kwetu kuishi maisha ya ukristo **(Waefeso 4:1)** kwa sababu tumebarikiwa na hayo yote yametajwa maisha yetu yatakuwa tofauti.
- Maisha yetu ya nafasi katika Kristo, yatabadilisha hali ya maisha yetu hapa duniani.
- Awali, kuishi maisha ya ukristo hakungewezekana, lakini sasa kwa sababu ya baraka hizi zetu za kiroho ndani ya Kristo kunawezekana.
- Hapo mwanzo, tuliishi duniani tukiongozwa na dhambi, kifo lakini Mungu alituokoa na nguvu zake na tulizaliwa katika familia yake. Alituvisha na utukufu wake na ametupa urithi sawa na mwanawe Yesu Kristo.
- Sasa vile tunajua maisha yetu yamebadilishwa hivi, inatupasa tuamini ukweli na tusirudi nyuma kwa kuishi vile tulivyoishi kabla ya Yesu kutuokoa.
- Kwa neema ya Mungu, sasa tuko katika familia ya Mungu na ametupa nguvu na tamaa kuishi maisha yetu yakiwa na thamani ya ile neema ya ajabu, na huruma ambayo imewekwa kwetu.
  (Warumi 12:1-2)

B. **Kutembea kwa thamani.**

[2] Kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uvumilivu, mkichukuliana katika upendo; [3] na kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani. **(Waefeso 4:2-3)**

- Kutembea ambako kunathamani ya nafasi yetu mpya au kuitwa ni kutembea kwa unyenyekevu. Tunaona hali yetu iliyo ovu mbele ya Mungu na vitu vyote tunavyo na maisha yetu yote yanatoka kwake
- Tena ni kutembea kwa upole, upole unamaanisha “nguvu chini ya uongozi.”
- “Kuteseka kwingi” ni kutembea ukiwa na utulivu na kutumainia na kupumzika na kutegemea Mungu kutupatia nguvu na tama kuwa na utulivu na uvumilivu na wengine.
- Kutupatia nguvu kuishi maisha yenye thamani ya mwito wetu ambao inapatikana katika Warumi 6. Mpaka tujue na kuamini kwamba mwili wetu umeshulubiwa na Kristo na kwamba tumefufuliwa kutembea kwa maisha mpya.
- Tumepewa maisha halisi ya Kristo kama yetu, ukubali hayo kama ukweli.
- Tukiwa tunategemea Roho mtakatifu kufanya kazi yake ya kutuonyesha kiwango cha ukuaji, maisha ya Kristo ambayo tumepewa **(Yohana 16:13-14**) kwa imani tutayakubali na yatakuwa kitu cha kweli katika maisha yetu. (**2 Wakorintho 3:17-18)**

C. Kifungo cha amani.

3 ***Na kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani.*** (**Waefeso 4:3)**

- Tazama kwamba mstari huu hausemi “umoja wa mwili” bali ni “umoja wa Roho” hatujaambiwa tuzalishe umoja huu ni kitu ambacho Roho Mtakatifu amekamilisha.
- Tazama kwamba umoja huu, ambao unazaliwa na Roho mpaka udumishwe “ndani” kifungu cha amani, tukitia maanani kwamba amani ni matunda ya Roho.
- Tukiishi katika Roho, na Roho mtakatifu anazalisha amani katika maisha yetu ni amani hii ambayo itadumisha umoja kati ya ndugu.
- Tukitembea katika Roho, na matunda ya amani yanadhihirishwa katika maisha yetu, tutakuwa na uwezo wa kuzungumza na wengine katika hali yoyote kwa njia isiyo na mgongano, mvutano, au kushambuliana.
- Tutakosana na kuhimizana na kupatia wengine changa moto kwa njia ya amani, kwa upendo, na kuchukua jukumu la wengine moyoni.
- Umoja wa Roho mtakatifu mwishowe utadumishwa naye tukitembea katika Roho.
- Ni umoja wake kuudumisha.

D. Mwili mmoja, Roho, tumaini, Bwana, Imani, Batizo Mungu na Baba

4 Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. 5 Bwana mmoja, Imani moja Ubatizo, mmoja 6 Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote **(Waefeso 4:4-6)**

- Kwa sababu ya tofauti ya imani yetu na mafundisho, wakati mwingine ni rahisi kufikiri kwamba tunafaa kutengana na makundi mengine yasiyoonekana sio kama sehemu moja ya mwili wa Kristo
- Mistari hii inaweka wazi kwamba waumini wote wana mwili mmoja, Roho mmoja , tumaini moja na Mungu na Baba mmoja.
- Mwili unatufanya tuelewe na kusikia maneno vibaya ambayo yanajenga na kudumisha vizuizi na tofauti ndani ya Kanisa (mwili wa Kristo.)
- Tukitembea kwa Roho, tunadumisha umoja wa Roho kati ya ndugu wengine, tukitumainia Roho kutuleta sote kwa ukweli, “Mwili mmoja na tuko ndani yake pamoja” “Roho mtakatifu mmoja” ambaye anafanya kazi ndani yetu na kupitia kwetu kwa lengo moja la kutukuza Mungu na kutuumba kwa sura yake “tumaini moja” ndani ya Kristo ambaye ni sigingi ya Roho zetu (**Waeb 6:19)** “Bwana mmoja” wa maisha yetu ambaye ametuweka kando tuwe mali yake na kututumikia **(Efeso 2:10) “**Imani moja” ndani ya Kristo na kwa kifo chake. (**Warumi 6:13)**
- Tunaweza kutumainia Mungu kwa imani na utulivu ambao kila mtoto halisi wa Mungu ni wake ingawa tuko na imani na dini tofauti

E. Karamu

[7] Lakini kila mmoja wetu alipewa neema kwa kadiri ya kipimo cha kipawa chake Kristo. [11] Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa wanabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; [1 2]Kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; [13] hata na sisi sote tutakapofikia umoja wa imani na kumfahamu sana mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamlifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo [14] ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu. (**Waefeso 4:7,11-14)**

- Kristo kwa upendo wake mzuri, kama kichwa na Bwana ndiye mpeaji wa karama.
- Tazama kwamba karama hizi tunapewa na Yesu anavyoona ni vyema.
- Karama hizi hatustahili kupata ama kuzipokea lakini tunazipata kwa neema pekee.
- Kwa maana hatustahili kupata hizi karama, au kuzipokea hakuna nafasi ya kujisifu ama kujiinua.
- Hebu tutazame karama ya kwanza iliyopewa kanisa; “Mitume”
- Hii ni karama ambayo ilipeanwa ili kuweka msingi ya Kanisa. Mungu alitumia mitume kuanzisha makanisa mapya na wakaandika, wakafundisha na kuweka imara neno lake kwa kanisa milele.

- Na tena Paulo ametaja manabii. Manabii wa Agano jipya walipeanwa na Mungu kulinda mwili dhidi ya walimu waongo ambao walikuwa wakati wa Paulo na bado wako hata wa leo.
- Inayofuata ni karama ya wainjilisti, muinjilisti ni yule ambaye ananguvu za ajabu na tamaa ya kueleza mambo ya Kristo kwa wengine.
- Karama inayofuata ni mchungaji, kazi yao ni kuongoza, kulisha na kulinda kanisa.
- Yesu ndiye mchungaji mkuu, lakini anapeana wengine Karama wawe wachungaji wa Kanisa.
- Walimu ni wale ambao wananjaa na kiu kwa ukweli wa kina wa neno la Mungu.
- Roho ikiwaonyesha walimu ukweli; pia atatumia walimu kufundisha wengine.
- Na sasa Paulo anaeleza kazi za hizi karama.

[12] Kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu hata kazi ya huduma itendeke hata mwili wa Kristo ujengwe. (**Waefeso 4:12)**

- Alipeana karama ya mtume, manabii, wainjilisti, Pasta – walimu kwa kusudi la kukamilisha mahitaji ya watu wake ili wakue, wawe na nguvu, na kutumiwa naye kujenga mwili wa Kristo
- Karama hizi zilipeanwa kwa muda gani?

[13] Hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana mwana wa Mungu hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufikia kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo; (Waefeso 4:13)

- Mpaka sisi sote tuwe na umoja wa imani na kumfahamu sana Kristo.
- Mpaka maisha ya Kristo yawe kwetu kwa utimilifu.

F. Mwili wa Kristo.

***[14] Ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu. [15] Lakini tuishike kweli katika upendo wa kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa Kristo. (Wae*feso 4:14-15)**

- Kristo amempatia kanisa Roho mtakatifu ili kanisa likomae.
- Ishara na ushahidi moja wa Kanisa ambalo halijakoma ni fikira iliyo badilika na imani kulingana na yule aliye zungumza mwisho au kitabu cha mwisho walichokisoma.
- Il hali ishara ya Kanisa ambalo imekoma na kuendelea kua katika sura ya Kristo, ni yule ambaye ana imani kama mwamba, ndani ya Kristo na neno lake pia, na

nguvu ambazo zimepewa na Mungu, na tama ya kuzungumza kuhusu ukweli kwa upendo.

16 Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo. **(Waefeso 4:16).**

- Mwili wako ukikosa kiungo chake kimoja, je! Unaweza kutenda kazi kwa ukamilifu? La
- Ni sawa na mwili wa Kristo. Waumini wote pamoja wanaitwa mwili wa Kristo, na kutenda kazi vizuri na kufanya mapenzi ya Mungu mpaka tufanye kila kitu kulingana na njia za Mungu kwa umoja na kutumainia Roho mtakatifu
- Kama kila mmoja anavyofanya katika huduma yake aliyopewa na Mungu mwili wote utafaidika na kulishwa neno na kujijenga kwake.

WAEFESO KWA WAUMINI WANAO KUA- SOMO LA 6

A. Kutembea

[17] Basi nasema neno hili, tena nashuhudia katika Bwana, tangu sasa msienende kama mataifa waenendavyo, katika ubatili wa nia zao; [18] ambao; akili zao zimetiwa giza, nao wamefarikishwa na uzima wa Mungu, kwa sababu ya ujinga uliomo ndani yao, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao; [19] ambao wakiisha kufa ganzi wanajitia katika mambo ya ufisadi wapate kufanyiza kila namna ya uchafu kwa kutamani. (**Waefeso 4:17-19)**

- Mistari hii zinaeleza kuzama chini kwa fikira za mawazo yetu.
- Dunia imeshikwa na kitu, fikira za kidunia na tamaa kutafuta amani na furaha "kutembea kwa fikira tupu za mawazo" kuvifuata vitu havina thamani ambavyo havina thamani ya uzima wa milele
- Dunia mara kwa mara inaunda mipango na kujaribu kutimiza mahitaji yake wakitengana na Mungu.
- Lakini Mungu anapendelea kwamba mitazamo yetu idumu tukimtazamia badala ya kutumainia yale ambayo dunia inatupatia.
- Watu wakija katika imani ya uokovu mara ya kwanza, wanakuwa na furaha kuhusu Mungu badala ya kukubali neema na huruma yake. Unyenyekevu, kuwa upya na furaha, na upendo wakwanza waliokuwa nao mara ya kwanza unatoweka **(Ufunuo 2:1-4**)
- ***"- - - Kwa fikira tupu ya mawazo yao- - -"*** kuzama chini ya dhambi kunaanza kwa kutembea kwa fikira tupu ya mawazo yetu" (kufuatilia vitu havina thamini)
- Na Paulo anatuambia kwamba "kufahamu kwetu kutakuwa na giza" ghafla tu ukweli wa Biblia uliokuwa mazuri" na wakupendeza utakuwa na mawingu, kufichika, na usio na ladha.
- Baadaye "tunatoka katika maisha ya Mungu" hivyo Mungu hayuko katika fikira zetu.
- Kuondoka huku kutoka katika mawazo ya Mungu kutasababisha kurudi kwa "hisia za zamani" na kutaishia kwa kujikabidhi kwa kazi iliyo mchafu kwa tamaa mbaya (kuingia kwa dhambi yoyote wazi)
- Hii ndiyo ilifanyika kwa waisraeli jangwani walipoanza kutazama na kuweka macho yao kwa hali yao badala ya kutazamia Mungu. (**Kumb 6:10-11)**
- Mioyo yao ilikuwa na giza hawakuona ukweli ambao Mungu alizungumza na mwishowe hawakuwa na imani na wakafuatilia dhambi. **(Kumb 6:12)**

B. Mawazo mapya

[21] Ikiwa mlimsikia mkafundishwa katika yeye kama kweli ilivyo katika Yesu. (**Waefeso 4:21)**

- Mara tu kwa ghafla tazamo la Paulo liligeuka kutoka kwa taabu (Kuzama chini kwa dhambi) kwa usaidizi wa Mungu kwaYesu Kristo. Tazama Paulo, hasemi hujasoma kuhusu Kristo lakini anasema soma Kristo" Kusoma Kristo ni kumuelewa sio tu kujua kumhusu.

[21] Ikiwa mlimsikia mkafundishwa katika yeye, kama kweli ilivyo katika Yesu, [22] mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani unaoharibika kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya; [23] na mfanywe wapya katika Roho ya nia zenu; [24] mkavae utu mpya ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli. (**Waefeso 4:21-24)**

- Ukweli wa kwanza ambao tulisikia na kufundishwa kwa kudumu ndani ya Kristo na kutazama maisha yake unaanza katika mstari wa 22 " Mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani" tukipumzika katika kusulubiwa kwetu pamoja na Kristo " Mtu wa kale" anavuliwa nje ama kuwekwa kwa nafasi ya kifo na tunauwezo wa kutembea tukiwa huru kwa kutembea na kuongozwa naye.
- Ukweli mwingine tuliosikia na kufundishwa kwa kutazama Kristo ni kwamba mara "mtu wa kale" anatolewa nje, Roho mtakatifu anakuwa huru kufanya "mawazo yetu kuwa upya" Roho akianza kutazama maisha kwa njia za Mungu fikira zetu zitabadilika.
- Na mwishowe, tunaanza kuona maisha ya Kristo; Roho mtakatifu ataanza kuzalisha maisha ya Kristo ndani yetu (kuvaa maisha mapya)

[25] Basi uvueni uongo, mkaseme ukweli kila mtu na jirani yake; kwa maana tu viungo, kila mmoja kiungo cha wenzake. (Waefeso 4:25)

- Kwa hivyo, kwa sababu mtu wa kale ametolewa tunafaa tuishi tofauti (Mstari wa 25-32.)
- Kwa nini Paulo anasema kwamba tunafaa kusema ukweli kwa wenzetu? "kwa sababu sisi ni kiungo cha wenzetu"
  itakuwa ni ujinga kwa mkristo fulani kusema uongo kwa mwenzake, itakuwa ni kama mtu ambaye anadanganya nafsi yake.

[26] Mwe na hasira, ila msitende dhambi; jua lisichwe na uchungu wenu bado haujawatoka. (**Waefeso 4:26)**

- Wengine wanafundisha kwamba hasira zote ni dhambi, msitari huu unasema kwamba hasira zote si dhambi. Hasira inakuwa dhambi wakati gani na sio dhambi wakati gani?

- Kila kitu ambacho kinanipatia hasira ni kitu ambacho mtu amenifanyia vibaya, ni dhambi kwa maana mtazamo wangu uko kwangu.
- Yesu hakuwa na hasira kwa watu kutokana na vitu walivyomfanyia lakini hasira yake ilikuwa kwa vitu walifanya kinyume kwa Mungu.

***[27]Wala msimpe Ibilisi nafasi. (Waefeso 4:27*)**

- Mstari wa 26 unatuambia “jua lisichwe na uchungu” NK usiruhusu hasira yako iendelee mbele na mbele, kwa maana tukizidi kuwa na hasira ndivyo tuta zidi kuzama chini kwenye dhambi, na ndivyo tutaongozwa na shetani katika maisha yetu kupitia kwa mwili, tukitembea kwa mwili tunafanya vitu vya mwili (**Wagalatia 5:9-21**) wivu hasira, fitina, faraka uzushi).

[28]Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji. (Waefeso 4:28)

- Kabla ya kuokolewa, tunaweza tu kutembea kwa mwili, na kwa mwili tunazingatia tu nafsi yetu.
- Ubinafsi wetu ndani ya mwili unajionyesha kwa njia tofauti tofauti. Kwa wengine ni kuiba.
- Paulo anasema kwamba sasa kwa maana mtu wa kale ametolewa, na Roho mtakatifu anaweka mtu mpya, kuiba kwetu na kufanya vitu kwa njia isiyofaa unabadilishwa na bidii na kazi njema sio tu kwa faida yetu, na kwa mtazamo wa kusaidia wengine
- Ni kitu kingine, kufanya mwizi kuwacha tabia ya uizi, lakini ni kazi ya Roho mtakatifu kuzalisha maisha ya Kristo ndani yetu ambayo itafanya mwizi kufikia katika mahali ambapo atawacha uizi kupata kazi na kupatia wengine.

***[29] Neno lo lote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia.* (Waefeso 4:29)**

- Sasa vile mtu wa kale ametolewa, mawazo yanakuwa mapya na mtu mpya (Kristo) mazungumuzo yetu yatakuwa tofauti. Sasa tunanguvu na tama kuzungumza maneno ambayo yatabadilisha mioyo kwa Kristo na kuhimiza wengine.

[30] Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi. (Waefeso 4:30.)

- Mtu wa kale amesulubiwa na Kristo, tumepewa hali yake, na pia Roho angetutia hali yake, na pia Roho mtakatifu kutuonyesha ukweli. Sasa tunaweza kuamini na kutembea kwa ukweli
- Kama hatutembei kwa imani na kumtumainia Kristo, tutamhuzunisha Roho mtakatifu.
- Tazama vile Paulo alivyoongea “mlitiwa mhuri hata siku ya ukombozi” Roho mtakatifu sio tu” mhuri wetu” kuonyesha tuko kwa Mungu (ni sawa na kuweka alama kwa farasi). Na matumizi ya neno “mhuri” ina maana ya kutufungia ndani na kutuweka salama. **(**Yohana 10:28-29).

[31]Uchungu wote na ghadhabu na hasira na kelele na matukano yaondoke kwenu, Pamoja na kila namna ya ubaya. (Waefeso 4:31)

[32] Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi. (Waefeso 4:32)

- Je, ume wahi kuwa na hasira kwa mtu kwa kujaribu kwa bidii kuzuia hasira na haiwezi kutoka?
- Ingawaje, sasa vile mtu wa kale amekwishatolewa, mawazo kuwa mapya na kuvaa mtu mpya kuna nguvu mpya na tamaa sio tu kukomesha hasira, Roho mbaya, mazungumzo mabaya, kuna mabadiliko makubwa (kutoka kwa ubinafsi kwenda kwa Kristo) na Roho nyepesi yenye upendo na ya kusamehe.

WAEFESO KWA WAUMINI WANAO KUA- SOMO LA 7

Kabla kuanza kusoma Waefeso 4, mpaka turudi kusoma **(Waefeso 4:17-24)** kwa vile Waefeso 5 ni maendelezi ya 4

17 Basi nasema neno hili, tena na shuhudia katika Bwana, tangu sasa msienende kama mataifa waenendavyo, katika ubatili wa nia zao 18 ambao; akili zao zimetiwa giza, nao wamefarikishwa na uzima wa Mungu, kwa sababu ya ujinga uliomo ndani yao, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao 19 ambao wakiisha kufa ganzi wanajitia katika mambo ya ufisadi wapate kufanyiza kila namna ya uchafu kwa kutamani. 20 Bali ninyi, sivyo mlivyojifunza 21 ikiwa mlimsikia mkafundishwa katika yeye kama kweli ilivyo katika Yesu, 22 Mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani unao haribika kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya 23 na mfanywe wapya katika Roho ya nia zenu 24 mkavae utu mpya ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli. **(Waefeso 4: 17-24)**

- Kwa sababu miili yetu imesulubiwa na Kristo na tumepewa maisha mapya, Paulo anaeleza kitu katika sura ya 4 ambacho kinafaa kiwe sehemu ya maisha yetu.
- Kwanza anasema kwamba tuseme ukweli kila mara.
- Ni heri tuwe na hasira kwa kila kitu ambacho kinaenda kinyume cha Mungu lakini hasira inayotazama nafsi yetu isiwe katika maisha yetu tukitembea kwa Roho.
- Hatuta patia shetani nafasi kufanya kazi katika maisha yetu
- Badala ya kuiba tutafanya kazi kutosheleza mahitaji yetu na kwa wengine pia.
- Maneno yetu yatakuwa ni ya kuhimiza yaliyo na ustaidizi kwa ukuaji wa wengine.
- Hatuta huzunisha Roho mtakatifu kwa kukosa imani
- Na tutazungumza na kutendea wengine kama vile Mungu ndani ya Kristo alitusamehe.

A. Ni heri watoto wamungu watembee kwa upendo

1 Hivyo mfuateni Mungu kama watoto wanaopendwa (Waefeso 5:1)

- "Ndiposa" neno linatazamia nyuma katika sura ya 4, kwa sababu ya yale yote Roho mtakatifu amefanya katika maisha yetu katika Efeso 4 sasa tunauwezo, kwake" kufuata Mungu kwa bidii.
  (**Zaburi 63:8.)**
- Maelezo "kama watoto wanaopendwa" kuna maana kufuatilia Mungu na imani kama mtoto.

B. Tumepewa sura (hali) ya /Mungu

[1] Hivyo mfuateni Mungu, kama watoto wanaopendwa [2] mkaenende katika upendo, kama Kristo naye alivyowapenda ninyi tena mkajitoa kwa ajili yetu, sadaka na dhabibu kwa Mungu, kuwa harufu ya manukato. (Waefeso 5:1-2).

- Paulo anasema kwamba kama watoto wa Mungu, tumepewa hali yake na mambo yote ambayo yanatokana na hayo.
- Yote yale Mungu anafanya yana pewa changamoto na pendo lisiloangalia nafsi yake, basi yote yale tunafanya yatahimizwa na pendo lake kama Roho mtakatifu anazalisha maisha ya Kristo ndani yetu.
- Tembea kulingana na hali yako mpya (Waefeso 3:17-19.)

[3] Lakini uasherati usitajwe kwenu kamwe, wala uchafu wo wote wa kutamani kama iwastahilivyo watakatifu [4] wala aibu wala maneno ya upuzi wala ubishi; hayo hayapendezi; bali afadhali kushukuru. [5] Maana neno hili mnalijua hakika, ya kwamba hakuna mwasherati wala mchafu wala mwenye tamaa, ndiye mwabudu sanamu, aliye na urithi katika ufalme wa Kristo na Mungu [6] mtu asiwadanganye kwa maneno yasio na maana, kwa kuwa kwa sababu ya hayo hasira ya Mungu hawajia wana wa uasi [7] Basi msishirikiane nao [8]Kwa maana zamani ninyi mlikuwa giza, bali sasa mmekuwa nuru katika Bwana enendeni kama watoto wa nuru [9] kwa kuwa tunda la nuru ni katika wema wote na haki na kweli [10] mkihakiki ni nini impendezayo Bwana. **(Waefeso 5:3-10)**

C. Sura mpya

- Vitu ambavyo havihitajiki kwa hali yetu mpya na vitu ambavyo wasio amini wanafanya kama tabia
- Ni katika hali yao kufanya vitu hivyo vile ilivyo kuwa katika hali yetu ya zamani na sio sasa.
- Tukimaliza kufanya kazi mchana mzima tutachafuka, tutapendelea kuwa hivyo?
- La. Tunaenda nyumbani na kuoga kwa sababu sio hali yetu kuwa na uchafu.
- Na ngurue wako namna gani? Wanapenda kuwa wachafu! Wataenda nje kutafuta uchafu mwingi. Ni hali yao kuwa wachafu.
- Kama vile hatupendelei kuwa wachafu, kama watoto wa Mungu hatutafuraia kuendelea kwa dhambi.
- Wakati mwingine tunaweza kuteleza na kuanguka hata kuasi na hatuta kuwa na furaha tukiendelea kuwa katika mwili kwa sababu sio hali yetu.
- Wasio amini wanapenda kutenda dhambi, kwa sababu ni hali yao
- Inawezekanaje tupatwe tukifanya vitu ambavyo watu wadunia wanafanya tutahukumiwa kwa hayo?

D. Kuwekwa kando

- Paulo anasema kwamba hali yetu ni tofauti, kwamba isiwe ni mzaha kufurahia katika njia za dhambi za wasioamini.
- Sisi pia tulikuwa watoto wa giza wasio jua ukweli na sasa tuko watoto wa nuru.
- Roho mtakatifu ametufunulia ukweli wa neno la Mungu na sasa tunajua yaliyo mema.
- Kwa hivyo itakuwa vibaya kwetu kwenda nyuma na kutembea kama watu walioko kwenye giza wasio jua ukweli.
- Tukitembea tukitumainia Roho mtakatifu, atatuwezesha kufanya yaliyo mema, na kumpendeza Mungu.
- Mstari wa [10] unatuambia tusome yaliyompendeza Mungu. Ni kitu gani kinachomfurahisha Mungu? (**Waebrania 11:6)**
- Hivyo tunaona kwamba “Bila Imani” “hatuwezi kumfurahisha Mungu.
- Kama hatujakubali na kutumainia Mungu hatuta mpendeza Mungu

[11] “Wala msishirikiane na matendo yasiozaa ya giza, bali myakemee; [12] Kwa kuwa yanayotendeka kwao kwa siri, ni aibu hata kuyanena [13] Lakini yote yaliyokemewa hudhihirishwa na nuru maana kila kilichodhihirika ni nuru. [14] Hivyo kusema Amka, wewe usinziaye, Ufufuke katika wafu,Na Kristo atakuangaza. (Waefeso 5:11-14)

- Hapa Paulo anatuambia kwamba sio tu kuwacha kujiusisha na matendo maovu ya watu wasio amini, bali tunastahili kuonyesha dhambi zao.
- Tunaweza kuonyesha dhambi yao namna gani?
- Kwa maisha yetu. Tukitembea tukitumainia Roho mtakatifu maisha yetu yatazalisha matunda ya Roho Mtakatifu **(Wagalatia 5:22,23)**
- Watu wakiona matunda ya Roho mtakatifu yakizalishwa ndani na kupitia kwetu, wanaweza kushawishika. Baada ya kusawishwa wengine watakuja kwa Bwana kwa uokovu.
- Kwa nini Abeli aliua Kaini? Je, Abeli alimwambia Kaini kwamba alikuwa anakosea Mungu? Hapana, Abeli kutenda yaliyo kuwa mema yalishawishi Kaini kwamba hakufanya vizuri.
- Tukitembea tukitumainia Roho mtakatifu atatumia maisha yetu kwa njia hiyo.
- Wamisonari wakienda katika eneo jipya. Wanaenda nje na kuambia watu kwamba wao ni wenye dhambi na Roho yao inaabudu kwa dhambi?
- Hapana, wanafundisha tu neno la Mungu na watu wakisikia ukweli Roho mtakatifu anahukumu Roho zao kuhusu, vitu hivyo.
- Hatuhitaji kutaja dhambi za watu na tukitembea tukitumainia Roho mtakatifu atatumia vitendo na maneno yetu kufanya kazi katika maisha ya wengine kwa mapenzi yake.

[18] Tena msilewe kwa mvinyo ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho. (Waefeso 5:18)

- Katika **Waefeso 5 :18** Paulo alisema kwamba waumini wote wanafaa waongozwe na Roho. Na kuanzia mstari wa 22 Paulo anazungumza kuhusu uhusiano mbali mbali, mme/ mke mtumwa/ Bwana mzazi/ mtoto.
- Kwa kusoma uhusiano, na vile tunafaa kutende wenzetu, tuweke maanani mstari wa 18.
- Ndiyo njia ya pekee tunaweza kuenenda kwa husiano kama Paulo alivyo andika hapa kwenye kitabu cha waefeso itakuwa kutembea kuongozwa na Roho.
- Kabla hatujasoma kitabu cha Waefeso ingekuwa vizuri kwetu tuangalie nyuma kwanza mfano wa mme/ mke ndoa ya kwanza ilianza wapi? Ilikuwa ni fikira ya nani?

A. Mahitaji ya Adamu

***[19] Bwana Mungu akafanyiza kutoka katika ardhi kila mnyama wa msituni, na kila ndege wa angani, akamletea Adamu ili aone atawaitaje; kila kiumbe hai, jina alilokiita Adamu likawa ndilo jina lake [20] Adamu akawapa majina yao kila mnyama wa kufugwa, na ndege wa angani, na kila mnyama wa mwituni; Lakini hakuonekana wa kumsaidia Adamu aliyefanana naye. (Mwanzo 2:19- 20*)**

- Kwa nini Mungu alifanya Adamu kuwapa majina wanyama? Pengine kumwonyesha mahitaji yake. Pengine Adamu hakufikiria kwamba hakuwa na msaidizi mpaka alipoanza kupatia wanyama majina na kuona kwamba wote walikuwa na wasaidizi, wacha tuangalie vile Mungu alimpatia Adamu mahitaji yake ya mke.

  ***Bwana Mungu akamletea Adamu usingizi mzito, naye akalala kisha akatwaa ubavu wake mmoja, akafunika nyama mahali pake [22] na ule ubavu alioutwaa katika Adamu Bwana Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu.* (Mwanzo 2:21-22)**

- Kuna vitu vitano Mungu alifanya hapa kupitia Adamu usingizi; kuchukua ubavu kufunika nyama; kutengeneza mwanamke; kumleta kwa Adamu.

B. Mungu alimfanyia Adamu kulala

- Mungu hakuhitaji usaidizi wa Adamu Mungu ndiye aliamua vile mke wa Adamu angekuwa Adamu hakuamka kutoa pendekezo lake.

C. Mungu alimfanya Adamu kulala

- Kwa nini ubavu? Mbona hakuchukua sikio au mguu au nywele?
- Ubavu ni sehemu ya kando ya Adamu, Eva hangekuwa “Kichwa” cha Adamu na kuwa juu yake au kuwa chini yake, angekuwa sawa naye.
- Ubavu ulikuwa karibu na moyo. Eva angekuwa karibu na moyo wa Adamu kwa upendo na ulinzi.
- Ubavu ulikuwa karibu na moyo wake angehitaji ulinzi wa Adamu kila mara vile kuku analinda vifaranga wake kwa mabawa.

D. Mungu alifunika nyama

- Sio kama kufanyiwa operesheni siku hizi, hakuhitaji muda wa kupona.

E. Mungu aliumba mwanamke

- Ilikuwa ni kazi ya Mungu.

F. Mungu alimleta kwa Adamu

- Mungu alikuwa anataka Adamu ajue kwamba alikuwa ni zawadi kutoka kwa Mungu mwenyewe.
- Ni Mungu ndiye alianzisha ndoa. Ndoa ni uvumbuzi wa Mungu sio wa binadamu.

G. Mwanamke kumtii mumewe

22 Enyi wake, watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu 23 kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha kanisa; naye ni mwokozi wa mwili 24 lakini kama vile kanisa limtiivyo Kristo vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo. **(Waefeso 5:22-24)**

- Paulo anaanza kusema kwamba wake wawe chini ya waume wao vile wangekuwa chini ya Bwana.
- Mungu alimweka mume kuwa kichwa cha mwana mume 1Wakorintho 11:3) na pia mpeaji na mlinzi wake kwa hivyo mpaka atii mamlaka ambayo Mungu ameweka juu yake.
- Mstari wa 24 unaeleza vizuri kwamba mwanamke mpaka atii mumewe kwa kila jambo. Je kama jambo hilo ni kinyume cha neno la Mungu?
- Matendo ya mitume yanatukumbusha, wakati wafarisayo waliwaamuru.

- (**Mitume 5:28-29)** ni hivi, wake mpaka watii waume wao kwa kila jambo isipokuwa likienda kinyume na neno la Mungu.

H. Wanaume wapende wake wao.

[25] Enyi waume, wapendeni wake zenu kama Kristo naye alivyopenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake [26] ili makusudi alitakasa na kulisafisha kwa maji katika neno [27] apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na ila wale kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa. [28] Vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe. Ampendaye mkewe hujipenda mwenyewe [29] maana hakuna mtu anayeuchukia mwili wake popote; bali huulisha na kuutunza, kama Kristo naye anavyolitendea kanisa [30] kwa kuwa tu viungo vya mwili wake. **(Waefeso 5:25-30)**

- Paulo anaamuru wanaume kuwapenda wake zao kama vile Kristo alivyo penda Kanisa.
- Tuende nyuma katika shamba la Edeni, kwa Adamu na Eva.
- Alitoka katika karibu na moyo wake kwa upendo na ulinzi.
- Baada ya Mungu kumleta Eva kwa Adamu tazama vile Adamu alivyo sema mara moja **(Mwanzo 2:23)** Eva mara moja
- Kwa wakati huu, Eva alifanya chochote ili Adamu ampende? Hapana.
- Nani Adamu alimjua vyema, Mungu au Eva? Mungu. Alikuwa hajaona Eva hapo awali.
- Kwa hivyo, ni kitu cha muhimu kuona kwamba Adamu kumkubali Hawa ilikuwa kulingana na uhusiano wake na Mungu.
- Adamu alitosheka na pendo la Mungu kwake, na alijua kwamba Mungu angempatia kitu kizuri kwa hivyo alimkubali Eva mara moja.
- Hata sisi ni heri tuwakubali wake zetu na kuwapenda kwa maana Mungu anatupenda na alitupatia wake hao sio kwa ajili ya tabia yao.
- Na sasa inawezekanaje wake kutii na kuheshimu waume wao, na inawezekanaje waume kuwapenda na kuwakubali wake zao vile Paulo anavyo tuamuru?
- Tukijazwa na Roho mtakatifu vile tunavyo soma katika mstari wa 18.
- Tukiamini kwamba miili yetu imesulubiwa na Kristo na tumepewa hali mpya na tegemeo letu ni Roho mtakatifu tutawezeshwa kuishi kulingana na hali yetu mpya ambayo itatii neno la Mungu.
- Mwanamke ambaye anatembea kwa mwili hawezi kutii mumewe.
- Yeye atatazama tu makosa yake na ataasi mamlaka yake.
- Lakini mwanamke ambaye anatembea kwa Roho atazama na tegemeo lake liko katika Mungu sio kwa mumewe **(Isa 26:3**)
- Anaujasiri katika pendo la Mungu kwake ili kwamba ingawa mumewe anafanya makosa, Mungu atatumia hayo kwa wema kwa ajili yake.

- Kwa hivyo yuko na uhuru kumtii mumewe.
- Paulo aliwaamuru wanaume kupenda wake zao kama vile Kristo alivyopenda Kanisa.
- Hii haiwezekani kwa mume ambaye yuko kwa mwili.
- Kwa vile mume ambaye yuko kwa mwili atalinda tu mwili wake na mahitaji yake. Hatajali mahitaji ya wengine hata mkewe.
- Lakini mtu ambaye yuko kwa Roho tazamo lake litakuwa kwa wengine kuwa muhimu kuliko yeye. (**Wafilipi 2:3,4)**
- Nia yake kubwa itakuwa nikuona kwamba mkewe anapokea vitu vile anavihitaji.
- Kumbuka kwamba Mungu alimuumba Eva kutoka kwa mwili wa Adamu, alikuwa sehemu ya mwili wake.
- Kwa hivyo katika (**Waefeso 5:28-31)** Paulo anawaamuru wanaume kupenda wake zao na kuwalinda kama vile wanaweza kulinda miili yao.
- Uki kata mkono wako, unaweza kumwambia mkono wako, “wewe una ujuzi vile ninakutaka uwe” Sitajali hata kama utapona kwa hivyo sita kulinda.”
- Hapana huwezi kusema hivyo, kitu kikifanyika kwa mkono wako kitadhuru mwili wako wote.
- Huwa tunafanya nini wakati wake zetu hawafanyi yale tulitarajia wafanye?
- Tunakuwa na hasira na tunawakataa. Tunatazamia nafasi nzuri ili tulipe kisasi, Paulo anasema kwamba tuko na mwili mmoja na tunge wapenda na kuwalinda wake zetu sio kwamba wanafanya kila kitu vizuri lakini kwa sababu ni sehemu ya miili yetu tumepewa na Mungu.

I. Watoto

[1] Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki. [2] Waheshimu baba yako na mama yako; amri hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi [3] Upate heri ukae siku nyingi katika dunia. **(Waefeso 6:1-3)**

- Watoto ambao ni waumini mpaka waongozwe na Roho.
- Watoto ambao wanatembea kwa Roho watatii wazazi wao na wale ambao wanatembea kwa mwili hawata tii wazazi.
- Kwa sababu Mungu anawaamuru watoto kutii wazazi kwa hivyo wakikosa kutii wanaenda kinyume cha Mungu.
- Weka maanani kwamba kutii wazazi ni nusu ya yale Mungu anaamuru watoto mpaka wafanye hayo kwa Roho safi “mheshimu baba na mama..”
- Tazama Paulo anatuambia kwamba hii amri ina ahadi inayo shikana naye “ili iwe wema nawe na uishi miaka mingi duniani.”
- Ni vipi vile, watoto wakikosa kutii wazazi na kukosa kuwaheshimu uhusiano kati ya mzazi na mtoto utazuiliwa na maisha yatakuwa magumu kwa mtoto. **(Methali 13:15)**

- Na zaidi Paulo anasema “ili uishi na kutohesimu wazazi kuenda kinyume cha mawaidha yao yenye busara kutakuwa na mikasa, ambayo itafanyika kwa kukataa kurekebishwa na wazazi, kwa wakati mwingine inaweza kuwa hata kifo cha mtoto. Mfano mzazi anamwambia mtoto asipande mti fulani, mtoto akikosa kutii, tawi likavunjika na mtoto akaanguka akafa angalia. **(Methali 30:1)**

J. Wazazi

6 “Nanyi, akina baba, msiwachokoze watoto wenu; bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana.”Waefeso 6:4

- Paulo anazungumza na akina baba ambao mpaka wajazwe na Roho Mtakatifu ili walee watoto wao “kwa hali na maonyo ya Bwana”
- Mara kwa mara, tunashughulikia mahitaji ya watoto wetu kwa njia ya kimwili, ambayo utafanya mwili wao kuwa na tamaa ambayo baadaye huleta hasira na uchungu.
- Wazazi ambao wanalinda watoto wao kupita kiasi na kukosa kuwapatia uhuru ili wapate kuanguka katika mienendo yao, mara kwa mara hawana subira, wana mahitaji mengi,
- wanaongea ovyo ovyo na wana kiburi, badala ya kuwa na mapenzi na kuwa wangalifu. Wazazi wale ambao huogofya watoto wao na kuwarudi watoto kwa hasira wanafanya watoto wao wakue wakiwa na hasira badala ya kuwa na upendo na mapendo mema. (Waeb 10:24)
- Wazazi wakiendelea kua kwa neema na neno la Kristo na kujazwa na Roho mtakatifu na maisha ya Kristo. Roho Mtakatifu atawawezesha kwa mifano mema kuwa watoto wao kufwata.
- Tena, tujue kwamba ni Roho mtakatifu ndiye atatuwezesha kuwafundisha na kuhimiza watoto wetu kila siku kutokana na ukweli wa neno la Mungu.
- Tena zaidi, kama sisi akina baba na akina mama tukitembea kwa Roho, Roho Mtakatifu atatuwezesha kufundisha watoto wetu, tukiwa mifano kwao, tukitembea kwa Roho na sio kwa mwili.
- Tukitembea kwa mwili, tutawafundisha watoto wetu kufanya hivyo (Johana 3:6)

K. Wabwana na Watumwa

“ Enyi watumwa watiini wao walio bwana zenu kwa jinsi ya mwili, kwa hofu na kutetemeka, kwa unyofu wa moyo, kana kwamba ni kumtii Kristo; wala si kwa utumwa wa macho tu kama wajipendekazao kwa wanadamu bali kama watumwa wa Kristo, mkitenda yampendezayo, Mungu kwa moyo kwa nia njema kama kumtumikia Bwana wala si mwanadamu; mkijua ya kuwa kila jema alitendalo mtu atapewa lilo hilo na Bwana kwamba ni mtumwa au kwamba ni huru. (Waefeso 6:5-8)

- Wakati Paulo aliandika kitabu cha Waefeso, lilikuwa ni jambo la kawaida kuwa na mabwana na watumwa wao. Wakati huu jamii yetu inatumia waajiri na waajiriwa.
- Fikira ya Paulo hapa ni kwamba waajiriwa ambao wanatembea wakiongozwa na Roho mtakatifu atamfanyia mwajiri wake kazi kama vile anamfanyia Bwana.
- Atafanya tu kazi kwa bidii wakati mwajiri wake anamtazama, na baadaye kuwa mvivu wakati hayuko karibu! kwa maana sisi ni watumizi wa Mungu yanatupasa tufanye kazi na mioyo yetu yote kama vile tunamfanyia Kristo.
- Mwajiriwa ambaye anatembea kwa mwili hatajali tu juu ya maisha na mahitaji yake, hatafikiria kumfanyia mwajiri wake kazi nzuri.
- Paulo anaendelea kusema kwamba zawadi yetu ya kweli haitoki kwa mwajiri na mwishowe itatoka kwa Bwana.

9 Nanyi akina bwana, watendeeni wao yayo hayo, mkiacha kuwaogofya, huku mkijua ya kuwa yeye aliye Bwana wao na wenu yuko mbinguni, wala kwake hakuna upendeleo. (Waefeso 6:9).

- Paulo sasa anazungumza na waajiri kuwakumbusha kwamba watendee waajiri wao vyema kwa upendo na kuwajali.
- Waajiri wakumbuke wao sio muhimu sana mbele ya Mungu kuliko walioajiri, na kwamba Mungu anatuona sawa.
- Kwa hivyo, kwa sababu mwajiriwa ndiye Mungu anampenda ni heri atendewe vyema.

- Wakati Paulo aliandika barua hii kwa waumini wa Efeso, alikuwa mfungwa katika Roma, mkono wake mmoja akifungwa na minyororo. Wakati wa Paulo, kulikuwa na wanajeshi wa Roma. Wanajeshi hawa walikuwa na silaha ya kuvaliwa kuwakinga. Kwa kawaida kitu cha kwanza mwanajeshi kuvaa ni mshipi katika kiuno chake. Mshipi huu ulikuwa wa muhimu sana kwa sababu vitu vingine vyote vilishikwa na mshipi, kinachofuata ni kisahani cha kifua, ilifunika kifua na mgongo wake na kuunganishwa kwa misipi, baadaye ali vaa viatu vya wanajeshi wa Roma zilitengenezwa na ngozi ya mnyama na sehemu ya chini kukamatwa. Pamoja na misumari. Baadaye mwanajeshi angechukua Sime yake.
- Katika somo letu la Waefeso leo, Paulo anatuonyesha kwamba sisi ni wanajeshi wa Kristo wanaozuia adui , Kama wanajeshi wa Roma walikuwa na nguo za kuwakinga na silaha kwa vita vyao hivyo basi Paulo alisema kwamba Mungu anawapatia Wakristo silaha na nguo za kujikinga kwa vita.

A. Vita yetu

[10] Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uwezo wa nguvu zake. [11] Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za shetani. [12] Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa Roho. [13] Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana Waefeso 6:10-13

- Leo kama watoto wa Mungu tuko katika hali moja kama waisraeli walivyo jikuta walipo toka huko misri.
- Walikuwa huru kutoka kwa uongozi na mamlaka ya wa msiri na katika ziwa Farao alikuja tena kuwateka.
- Kwa njia hiyo tumewekwa huru kutoka kwa nguvu za shetani lakini anaendelea kujaribu kudanganya watu kwa minajili ya kuwaongoza tena.
- Hawezi tena kututeka na kutuweka wake lakini kupitia kwa uongo anaweza kushawishi fikira, nia na hisia zetu na mwishowe kutuongoza.
- Nia kubwa ya Shetani ni kutudanganya ili tusiamini ukweli ulioko katika Warumi 6, ambao tukikosa kuamini utatufanya tuzidi kutembea kwa mwili.
- Hivyo tukiwa kwa mwili, Shetani anaweza kuweka fikira zetu ziwe mbali na Mungu kwa majaribio ya dunia hii.
- Kama vile Waisraeli hawangejilinda wenyewe kutoka kwa wa Misiri, hata sisi hatuwezi kujilinda kwa uongo, majaribio na mashtaka ya Shetani.
- Kwa hivyo Paulo anatuandikia mwishowe “ndugu zanguni muwe imara kwa Bwana na kwa nguvu ya ukuu wake. Kuvaa silaha zote za Mungu.

- Kwa nini ni muhimu kuwa imara katika bwana na ndani ya nguvu ya ukuu na kuvaa silaha zote za Mungu? Anatuambia sababu kwa sehemu ya mwisho wa mstari wa 11. Mpate kuweza kuzipinga hila za shetani, na tena Paulo anaendelea mbele kutuambia kwamba vita hii ni vibaya kuliko vita vyote tumewahi kuona.
- Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama, bali ni juu ya falme na mamlaka juu ya wakuu wa giza, juu ya majeshi
  ya pepo wabaya katika ulimwengu wa kiroho. Hatuwezi. kujilinganisha na maadui hawa hatuwezi kuona hata kitu ambacho tunapigana nacho, kwa hivyo mpaka tuwe imara kwa Bwana na kwa nguvu ya ukuu wake na kuvaa silaha zote za Mungu.
- Ni kitu cha kupendeza kutazama vile Paulo alivyotumia neno “kusimama” mahali hapa katika mstari wa 11 anasema vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani. Tukizipinga kwa kusimama kwa silaha. Katika mstari wa 13 anasema tena vaeni silaha zote za Mungu mpate kushindana siku ya uovu (kushindana tukisimama kwa Mungu) na mkisa yafanya hayo yote kusimama.
- Kwa lugha ya Grik neno ‘simama’ lina maanisha kuwa pahali tayari pame chukuliwa, na kazi yetu ni kuwa tu mahali pale, lakini namna gani?
- Katika 1 Petero 5:8-9 Petero aliandika “muwe na kiasi na kukesha, kwa kuwa mshitaki wenu ibilisi, kama simba angurumaye huzunguka zunguka akitafuta mtu ammeze” wale ambao wanamzua kwa bidii ni wale ambao wanasimama zaidi kwa imani.
- Hivyo basi tunaweza kusimama mahali petu namna gani kuzipinga hila za ibilisi? Kwa kumzuia kwa bidii kwa imani kwamba yeye ni adui ambaye tayari ameshindwa.**(**Wakolosai 2:15)
- Tazama nyuma kwa Waefeso 6:13 Paulo hatuambii kuchukua silaha na kuenda kunyakua Shetani.
- Hatuhitajiki kunyakua Shetani kwa sababu Yesu tayari alishafanya hayo.
- Kitu ambacho tumebakiwa kufanya ni kupumzika ndani na kuamini kwa ushindi kupumzika ndani na kuamini kwa ushindi ambao tumepewa.
- Mpaka tujifiche ndani ya Yesu, ushindi wetu kwa imani.
- Hivyo basi nini silaha ambayo Mungu ametupatia? Ni Bwana Yesu Kristo.
- Vile imetajwa awali Yesu tayari ameshinda Shetani na malaika wake wachafu na wako chini ya mamlaka yake.

siku ya uovu na mkiisha kuyatimiza yote kusimama (Waefeso 6:10-13)

- Kwa hivyo mpaka tujifiche ndani ya Kristo.Yeye ndiye silaha ye Mungu ambaye ametupa.

B. Ukweli

[14] Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani. **(Waefeso 6:14**)

- Ni kitu cha kupendeza kusoma **Yohana 14:6** kwamba Yesu alisema “Yesu akaamwambia, mimi ndimi njia na kweli na uzima; mtu haji kwa baba ila kwa njia ya mimi.
- Kwa hivyo mjifunge ukweli viunoni mpaka tuvae Bwana Yesu Kristo.
- Ukweli kuhusu Yesu, hali yake, mpaka ijulikane na kueleweka, mpaka tuwe na uhusiano wa kindani na mpaka tumjue Kristo
- Kumjua Kristo ndio ukanda ambao utashikanisha vitu vingine vya silaha pamoja.
- Baadaye inakuja “dirii ya haki” katika 1 Korintho 1:30 Paulo anatuambia kwamba Kristo ndiye haki yetu mpaka tuvae nafsi mpya **(Efeso 4:24)** Bwana Yesu Kristo.

C. Amani

[15] Na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani (**Waefeso 6:15)**

- **Wakorintho 15:1- 15** inaeleza “injili” ni kifo na kufufuka kwa Yesu Kristo. Kwa hivyo kama miguu yetu itakuwa tayari kwa injili mpaka tuvae Bwana Yesu Kristo.
- Tunaamini kwa Mungu, hata ingawa watu na shetani wanaweza kusema vitu kutuhusu, kwa sababu Bwana Yesu alikufa kwa dhambi zetu na kufufuka kutoka kwa wafu.
- Tunaweza kusimama imara kwa amani ya Mungu.
- Shetani atafanya kila kitu kutufanya kukosa kuona amani ambayo tunayo kwa Mungu na kutufanya tuwe na wasiwasi na kushangaa kama Mungu anatupenda na kutukubali kweli.
- Kama Shetani anaweza kutufanya kuamini uongo wake na kuwa na tashwishi na pendo la Mungu na kukubaliwa kwetu, hivyo basi tutapoteza utulivu na amani thabiti moyoni mwetu.

D. Imani

[16] Zaidi ya yote mkiitwa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima. Mishale yote yenye moto ya yule mwovu (Waefeso 6:16)

- Katika biblia yote, tunaona sehemu ya Mungu na sehemu yetu ndogo ya kuamini na tena sehemu ya Mungu. Mfano mzuri ni **Warumi 15:13** “***Basi Mungu wa tumaini na awajaze ninyi furaha yote na amani katika kuamini, mpate kuzidi sana kuwa na tumaini, katika nguvu za Roho Mtakatifu.*** “Tazama kwamba yote ni Mungu isipokuwa sehemu ya “Kuamini” ambayo ni sehemu yetu ndogo.
- Nyuma tena kwa **Waefeso 6:16** kwa msingi, Paulo anasema kuchukua ukweli (Kristo na kazi yake alimaliza msalabani). Tukisimama mbele ya Mungu tuko

wenye haki na amani) na tutaona ikituliza silaha ya Shetani iliyo kali ambayo ni kuwa na tashwishi.

E. Uokovu

[17] Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu. (**Waefeso 6:17)**

- Uokovu wote unahusu Yesu, kwa hivyo kuweka chapeo ya wokovu ni kuweka Bwana Yesu Kristo.
- Shetani anataka tukose kuona ukweli wa Warumi 6 kwamba mwili wetu umesulubiwa na anatufanya tuanze kujaribu kupigana na dhambi na nguvu zetu kwa sababu anajua hatuwezi kushinda.
- Ingawaje, tukishajua hakika kwamba Yesu alichukua pahali petu kwa kifo na kupakamilisha na vile kusulubiwa kwetu naye, alivyokamilisha tutaona ushindi juu ya dhambi na mwili.
- Ni kitu cha ajabu kuona mstari wa **14-17** umeunganishwa vizuri. Kwanza Roho mtakatifu atatufunga kiuno na ukweli ambao ni Kristo ambaye ni neno la Mungu linaloishi (alituweka ndani ya Kristo alituonyesha nafasi yetu mbele ya Mungu tukiwa wenye haki na tukiwa na amani inayo kamilika. Anatushawishi kuwa na wokovu unao kamilika kutoka kwa dhambi, kifo, shetani, na hukumu na kwa Mungu (Yesu Kristo) katika maisha yetu kutufanya kukua kwa neema na kuelewa Bwana Yesu Kristo.
- Maandishi ya kupendeza kufikiria hapa ni **Waefeso 4:20-21.**

F. Kuomba kila mara

[18] Kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote .(**Waefeso 6:18)**

- Neno kila mara kwa Grik (“Kuomba kila mara”) na Roho ni neno sawa linamaanisha pahali au nafasi iliyojulikana “Maelezo yake yanaweza kuwa “Kuomba kila mara” kwa sababu unakuwa katika nafasi au pahali panapojulikana pa kumtegemea Mungu na katika nafasi ya kuwa katika Roho.
- Kama Roho anatuongoza maishani, atatuongoza katika kumtegemea Mungu kila mara, maisha la kuomba kila mara. **1Thes 5:17**
- Ni vizuri kufikiria yafuatayo kuhusu neno ya maombi lililotolewa na John Darby, maombi ni njia kubwa ya kuweka, kujua kuwepo kwa Mungu, ni njia ya kuonyesha udhaifu wetu na kutubu mahitaji yetu kwake.
- Mara nyingine tunaona “silaha ya Mungu” maombi yanapata nguvu kwa Yesu Kristo.

G. Maombi kwa wandugu na wakina Dada

[19] Pia na kwa ajili yangu mimi, nipewe usemi kwa kufumbua kinywa changu ili nihubiri kwa ujasiri ile siri ya Injili. **(Waefeso 6:19)**

- Paulo anawaomba waumini waefeso kumwombea ili Mungu ampatie usemi na ujasiri kuihubiri Injili.
- Ni kitu cha kupendeza kuona kwamba wakati wa kuandika maombi ya kuombewa Paulo, alikuwa gerezani kwa ajili ya injili.

H. Tukiko

[21] Basi ninyi nanyi mpate kuzijua habari zangu, ni hali gani, Tikiko, ndugu mpendwa, mhudumu mwaminifu katika Bwana atawajulisheni mambo yote. ***(*****Waefeso 6:21)**

- Tukiko pengine ndiye alipeleka barua hii Efeso. Alikuwa mume ambaye alisafiri na Paulo na alimsaidia kufundisha neno la Mungu kwa makanisa ambalo yalianzishwa.
- [23] Amani na iwe kwa ndugu na pendo pamoja na imani zitokazo kwa Mungu Baba na kwa Bwana Yesu Kristo.
- Amani, upendo na imani inatoka tu kwa Mungu. Tukitembea kwa Roho tutaiona.

3217 Middle Road
Winchester, Virginia 22602
540-662-7743
fbc@fbcva.org
www.fbcva.org